Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 82 No. 237 | RAMAZ-SHAWAL.1444AH | APRILI 2023 | ZAHOOR 1402 HS | BEI TSH. 700/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Enyi mlioamini, si halali kwenu kuwarithi wanawake kwa nguvu; wala msiwazuie (kuolewa) ili mpate kuwanyang'anya baadhi ya vile mlivyowapa, isipokuwa wawe wamefanya uovu ulio wazi; na kaeni nao kwa wema ; na kama mkiwachukia, basi huenda mchukie kitu na AllahAmetia heri nyingi ndani yake. (An-Nisaa 4:20)

Ishara za ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa[as]

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu



Muhtasari wa Hotuba ya Ijumaa ya Hadhrat Ameerul Mumineen Mirza Masroor Ahmad Khalihatul Masih wa Tano[atba] iliyotolewa katika Masjid Mubarak, Uingereza siku ya Tarehe 24 Machi 2023

Baada ya kusoma Tashahhud, Ta'awwuz na Surah Al-Fatihah, Khalifa mtukufu, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (aba) alisoma aya ifuatayo ya Qur'ani Tukufu:

"Yeye ndiye Aliyemwinua Mtume katikawatuwasiojuakusoma,atokaye miongoni mwao, anawasomea Aya Zake na kuwatakasa na kuwafunza Kitabu na Hekima, na ingawa hapo kabla kwa hakika walikuwa katika upotevu dhahiri
Na kwa wengine miongoni mwao walio bado kuungana nao; na Yeye ni Mwenye ushindi kamli, Mwenye hakima."
(Qur'ani Tukufu 62:3-4).

Kuanzishwa kwa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba tarehe 23 Machi inajulikana ndani ya Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya kama Siku ya Masihi Aliyeahidiwa (as). Sisi tumebahatika kumkubali Masihi na Mahdi ambaye ujio wake ulikuwa kwa mujibu wa ahadi ya Mwenyezi Mungu. Mnamo tarehe 23 Machi 1889, Masihi Aliyeahidiwa (as) alipokea ahadi ya Baiat (kiapo cha utii) huko Ludhiana kwa mara ya kwanza na hivyo Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya ikaanzishwa.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba kuna matukio mbalimbali ambapo ujio wa Masihi Aliyeahidiwa (as) umebashiriwa, kama vile Aya za Sura ya 62 zilizosomwa mwanzoni, ambazo zinatabiri ujio wa mtumishi wa kweli wa Mtukufu Mtume (saw). Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba atawasilisha maelezo ya Aya hizo hapo juu pamoja na dalili mbalimbali za ujio wa Masihi kwa maneno ya Masihi Aliyeahidiwa (as) mwenyewe.

Ishara za Ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa (as)

Khalifa mtukufu (atba) umemnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba aya hizi zinaeleza kwamba Mtukufu Mtume (saw) alitumwa na Mwenyezi Mungu katika wakati ambapo watu walikuwa wamepotea kabisa na kuacha njia. Hivyo, kwa kumtuma Mtukufu Mtume (saw), watu hao waligeuzwa kutoka kwenye hali ya chini kabisa hadi katika hatua ya juu kabisa ya kumtambua Mwenyezi Mungu. Vile vile, aya hizi zinaonyesha kwamba wakati kama huo wa giza ungedhihirika katika siku za mwisho, ambapo watu wangekuwa hawana ujuzi na ufahamu. Wakati huo utakapofika, watu wa wakati huo wangeonyeshwa yale ambayo yalionyeshwa kwa Maswahaba wakati wa Mtukufu Mtume (saw); kwa maneno mengine njia ya matengenezo yao kupitia mtu atakayetumwa na Mungu. Huku akifafanua aya hizi hizi, Mtukufu Mtume (saw) aliweka mkono wake juu ya bega la Salman Farsi (Muajemi) (ra)

Endelea Uk wa 4..

Maulamaa Wawili wa lugha

Na.
Mahmood Hamsin Mubiru - Kiwalani Dar es Salaam



Uk wa 5..

Jamia Waadhimisha Siku ya Masihi Aliyeahidiwa[as]



Tarehe 23 march ni siku ya kihistoria katika jamaat Ahmadiyya ulimwenguni, ni siku ambayo kwa mara ya kwanza kabisa mwanzilishi mtukufu wa jumuiya ya waislamu waahmadiyya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad as wa Qadian alianza kuchukua baiat za wafuasi wake katika mji wa Ludhiana nchini India- yaani tarehe 23/03/1889.

Kwa ajili hiyo basi waahmadiyya ulimwenguni kote ifikapo tarehe kama hiyo kila mwaka huadhimisha siku hiyo kwa kufanya mikutano katika matawi yote kwa shabaha ya kumshukuru Allah na kukumbuka historia yetu ya kule tulikotoka,hapa tulipo na shabaha ya kule tunakoelekea. Katika tawi letu la jamia ,maadhimisho hayo yalifanyika siku ya Jumanne tarehe 21/03/2023 mgeni rasmi akiwa ni Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry Sahib Amir na mbashiri mkuu hapa nchini.

Hafla ilianza majira ya saa 5:00 asubuhi chini ya mwenyekiti Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhatt sahib Naib Amir na Mkuu wa chuo cha Jamia Ahmadiyya Tanzania.kama ada yetu hafla ilianza kwa usomaji

Ukurasa wa 8..

Ukinaifu ndani ya Ndoa uk. 03..

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Kuvunja misalaba na kuuwa Nguruwe

Tuna Imani isiyoyumba wala kutetereka kwamba Mtukufu Mtume Muhammad[saw] hasemi lolote. Ila kama inavyothibitisha Kurani Tukufu ***illa Wahyi huwa***.

Mbora wa viumbe wote ametupatia Habari za kutosha kuhusu Nabii Issa[as]. Kwa muhtadha wetu tunaangazia juu ya kauli kuwa akija atavunja misalaba na kuuwa Nguruwe. Uzuri wa mafundisho ya Islamu yameruhusu utumiaji wa akili. Hapana shaka kuwa atakuja, lakini atarudije yule ambaye Kurani Tukufu imetuhakikishia ya kwamba alikwisha kufa zamani, kwani siku ya Kiyama ataulizwa kuwa wewe ndiye ulifanya watu wakuabudu na Mama yako. Huyu mtumishi Mpole wa Allah. Atajibu uliponifisha wewe ndiye ulikuwa mlinzi, maana yeye hakurudi kuona watu wanavyo muabudu yeye na Mama yake. Kwahiyo hakupata fursa ya kurudi Duniani, lakini kitendawili ni kwamba atavunja Misalaba na kuuwa Nguruwe!

Hapa sasa ndipo panatakiwa balagha na mantiki. Lugha za waja wa Allah. Huwezi kuingia kwenye Ufalme wa Mungu hadi uzaliwe mara ya pili, kwanza ilitakiwa aje Eliya ndiyo John. Ni lugha hiyo hiyo itakayo tusaidia kuelewa maneno ya Mteule Mtukufu Mtume Muhammad[saw].

Ushahidi wa kifo cha Nabii Issa[as] umeelezwa kinagaubaga kwa kutumia hisitoria, Geografia, elimu ya utibabu katika kitabu cha Masihi Aliyeahidiwa, Hazrat Mirza Ghulam Ahmad[as] ***Yesu katika India***. Watafiti, wanahisitoria wanaofuatilia mambo ya Dini wao wanaandika juu ya kifo cha Nabii Issa[as] na alivyookolewa kutoka Msalabani. Kilele cha juhudi hizo ilikuwa ni mkutano wa kimataifa kuhusu kuokolewa kwa Nabii Issa[as] Msalabani. Wanasayansi, Wanahisitoria, mabingwa wa maswala ya Dini na wanasheria waliwasilisha utafiti wao. Kwa ujumla Nabii Issa[as] amefariki na tunamkumbuka mshairi aliyeomboleza ***Nabii Issa[as] afile, poleni bwana Padr.***

Lakini neno la Mtukufu Mtume Muhammad[saw] kuwa atarudi kuvunja Misalaba na Kuuwa Nguruwe. Huyu si Nabii Issa[as] aliyetumwa kwa Bani Israil, bali ni Nabii Issa[as] ambaye ni mfano wake. Ukitolewa wanaupigia kelele. Na Nabii Issa[as] wa mfano ambaye kwa amri ya Allah mwaka 1889 alianzisha Jeshi la kuvunja Misalaba na kuuwa Nguruwe. Jiunge na Jeshi hili ili kusimamisha umoja wa Allah. Kinachotakiwa ni kama anavyoshauri mshairi maarufu wa Kiswahili **Miyaka Bin Haji Al-Ghassaniy;-**

Muyaka
Imani bora Imani, tuwanile
Kwenda mbele
Mti wapukusha tunda,
waakasi okoteni
Na hatun a kizuizi chochote bali anawashangaa Rumi, ***Kwanini unaendelea kuwa gerezani wakati milango yote imefunguliwa?***



QUR'AN TUKUFU

وَلُوْطًا اِذْ قَالَ لِقَوْمِهٖۤ اَتَاْتُوْنَ الْفَاحِشَةَ مَا سَبَقَكُمْ بِهَا مِنْ اَحَدٍ مِّنَ الْعٰلَمِيْنَ ﴿۸۰﴾

Na (Tulimtuma) Luti alipowaambia kaumu yake: Je, mnafanya ufasiki ambao hajawatangulieni yeyote kwa huo katika walimwengu?

اِنَّكُمْ لَتَاْتُوْنَ الرِّجَالَ شَهْوَةً مِّنْ دُوْنِ النِّسَآءِ ؕ بَلْ اَنْتُمْ قَوْمٌ مُّسْرِفُوْنَ ﴿۸۱﴾

Hakika ninyi mnafika kwa wanaume kwa kuwaingilia badala ya wanawake, bali ninyi ni watu warukao mipaka!

وَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهٖۤ اِلَّاۤ اَنْ قَالُوْۤا اَخْرِجُوْهُمْ مِّنْ قَرْيَتِكُمْ ۚ اِنَّهُمْ اُنَاسٌ يَّتَطَهَّرُوْنَ ﴿۸۲﴾

Na hayakuwa majibu wa kaumu yake isipokuwa wakasema: Wafukuzeni katika mji wenu, maana hao ni watu wanaojifanya wametakasika.

فَاَنْجَيْنٰهُ وَاَهْلَهٗۤ اِلَّا امْرَاَتَهٗ ۖ كَانَتْ مِنَ الْغٰبِرِيْنَ ﴿۸۳﴾

Basi Tukamuokoa yeye na watu wa nyumbani mwake isipokuwa mke wake, alikuwa miongoni mwa wakaao nyuma.

وَاَمْطَرْنَا عَلَيْهِمْ مَّطَرًا ؕ فَانْظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُجْرِمِيْنَ ﴿۸۴﴾ ع

Na Tukawanyeshea mvua (ya adhabu). Basi tazama jinsi ulivyokuwa mwisho wa wakosefu (7:81-85)

NUKUU YA HADITHI

Hazrat Abu Huraira anasimulia kuwa yeye alimsikia Mtume saw akisema: Kiyama haitasimama mpaka jua lichomoke upande wa maagharibi na litakapochomoka na watu wataliona, wataamini wote ilhali haitafaa kwa nafsi yeyote Imani yake isiyoamini kabla yake.

Mwana Aliyeahidiwa[ra]

Na.
Mwandishi wetu.

Kama zilivyo taratibu za jamaati duniani kote, ifikapo Februari tarehe 20 kila mwaka , huadhimishwa siku ya mwana aliyeahidiwa r.a.

Jamia Ahmadiyya iliyo ni taasisi muhimu katika jumuiya, nayo haikubaki nyuma katika maadhimisho hayo adhwiim. Masheikh,waalimu,wanafunzi na hata kina mama na watoto walishiriki kikamilifu katika maadhimisho ya mwaka huu-2023. Hafla ilianza majira ya saa nne asubuhi (4:00) siku ya jumatatu chini ya uongozi wa mwenyekiti Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhatti sahib Naib Amir na mkuu wa chuo cha Jamia Ahmadiyya Tanzania kwa usomaji wa Qurani Tukufu iliyosomwa na ustaadh Ibrahim Ahmad Ngalombe na kufuatiwa na shairi la kiurdu ambalo lilisomwa na Ismail Abdullatif Pembe.

Baada ya shairi hilo,ulifuata usomaji wa bishara kuu ambayo ilisomwa na ustaadh Juma Mwanyika. Msomaji aliwakumbusha na kuwapitisha wahudhuriaji katika bishara adhwiim kumhusu Hadhrat Muslih Mau'ud r.a. Kama ilivyotolewa na Hadhrat Masihil mau'ud a.s tarehe 20/02/1886. Kisha ilifuata hotuba iliyokuwa na kichwa cha habari kisemacho, "Mipango mbalimbali na baadhi ya kazi za Hadhrat Muslih mau'ud r.a."mhutubu aliwaeleza mipango kabambe ya mwana aliyeahidiwa r.a ambayo imeleta maendeleo makubwa ya jamaat. Kwa uchache aligusia mipango kama vile; Tahrik – Jadiid, Waqfu-Jadiid n.k.

Baada ya hotuba hiyo ilifuata hotuba iliyobeba anwani isemayo, "Jinsi bishara zilivyotimia kwa mwana aliyeahidiwa a.s," iliyowasilishwa na Mwl. Shamuni Mwishehe Juma.

Mwalimu alijitahidi kudadavua kipengele kimoja baada ya kingine juu ya kutimia kwa bishara hizo katika dhati ya Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad[ra].

Baada ya hotuba hiyo ilifuata kaswida ya Masih mau'ud a.s iliyosomwa na Nasrullah-Masroor Ame na Twalha Mbanga. Baada ya qaswida hiyo ilifuata hotuba iliyochukua maudhui yasemayo, "Ahadi ya Hadhrat Muslih Mau'ud r.a wakati wa kifo cha Hadhrat Masihil Mau'ud a.s." Hotuba hiyo ilitolewa na Maulana Sheikh Abd-Nasir Baj-wa Sahib. Sheikh Sahib aliwaeleza wasikilizaji ile ahadi muhimu kabisa aliyotamka mwana wa ahadi wakati alipofariki baba yake mpendwa. Alisema kuwa mwana huyo alipokuwa na umri wa miaka 19 baba yake mpendwa yaani Masihi aliyeahidiwa a.s alifariki, yeye alisimama mbele ya maiti ya baba yake na kwa udhabiti mkuu alisema:- "Hata kama watu wa dunia nzima watakuacha, mimi nitaendelea kufanya juhudi hata kazi yako ikamilike." Sheikh sahib alifafanua mada hii na kutaja kazi mbalimbali alizofanya Hadhrat Mirza Bashiruddin Ahmad r.a kabla na baada ya kuchaguliwa kwake kuwa khalifa.

Baada ya hotuba hiyo zilifuata nasaha maalum za mgeni rasmi Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhatti Sahib, naib Amir na mkuu wa chuo cha Jamia Ahmadiyya nchini. Katika nasaha zake, Naib Amir sahib alinukuu sehemu ya aya kutoka katika suratul Luqmaan (31:35) isemayo "Allah huyajua yaliyomo matumboni ……"kisha alisema kuwa pamoja na maendeleo ya sayansi lakini kamwe haiwezekani kutambua mtoto aliye tumboni mwa mama atakuwa na sifa kadhaa wa kadhaa kama bishara zilivyobainisha kumhusu muslih mau'ud r.a kuwa atakuwa mwenye akili sana, atajulikana mpaka pembe zote za dunia , atakuwa sababu ya kukombolewa walio utumwani, atakuwa mtakatifu nk, ambapo haya yote yalibainishwa katika bishara hata kabla ya kuchukuliwa ujau zito miaka 3 kabla ya kuzaliwa kwake. Alisema kuwa bishara hii na kutimia kwake ni dalili tosha ya kuthibitisha ukweli wa Hadhrat Masih Mau'ud a.s. Mwisho mgeni rasmi aliongoza maombi ya kimya na kufunga hafla. Kisha washiriki walihudhuria katika sala ya adhuhuri na kushirki katika chakula cha pamoja.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe: 1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Ukinaifu ndani ya Ndoa

Na.



Maulana Sheikh Shaban A. Shunda

Takriban katika maisha ya wanandoa walio wengi kama sio wote, ndoa zao hupitia katika vipindi tofauti. Kama ulivyo umri wa Binadamu, ndoa hupitia katika kipindi cha utoto, ujana na uzee, na kila kipindi kina mambo yake na taratibu zake ambazo kama wanandoa watashindwa kuzifuata basi huenda ndoa hiyo ikakumbwa na mtihani mkubwa, nao ni mtihani wa kuchokana.
Kuna rafiki mmoja alisimulia kuwa alipooa katika siku zake za kwanza alikuwa alitoka bafuni kuoga na taulo analibwaga kitandani na mkewe kwa mapenzi hulichukua na kwenda kulianika nje, siku zilipozidi alianza kulikuta pale pale alipolibwaga na mwishowe kabisa aliambulia vichambo juu ya tabia yake hiyo. Hivyo ndoa ina madaraja na vipindi vya ukuaji wake, nitaelezea kwa ufupi huku nikijaribu kutoa dawa ya kumfanya bwana ndoa abaki kuwa kijana.

Utoto wa Ndoa

Wengine hukiita kipindi hiki (Fungate) mwezi wa asali, kipindi cha raha, utulivu, mapenzi, maelewano baina ya wanandoa. Si lazima kiwe mwezi mmoja au siku saba za fungate kama watu wengi wanavyoamini, bali kinaweza kikawa chini ya mwezi mmoja au zaidi ya mwezi mmoja au pia sawa na hali kisiwepo kabisa au pia kikadumu kwa mda mrefu.
Kwa mtu ambaye anataka ndoa yake idumu milele atumie kipindi hiki vizuri kusoma mazingira ya aliye naye kuwa yu mtu wa namna gani na sio tu kufaidi mambo mageni uliyomkuta nayo mwenzio na kufaidi kudekezwa.
Mtume[saw] alikuwa mara nyingine akija nyumbani kwake anamkuta mkewe kipenzi Hadhrat Aisha[ra] akicheza na midoli akiwa na wenziwe, naye alikuwa akimuacha aendelee na kujikalia pembe moja kuendelea na maswala yake.

Sayyidna Ahmad[as] ndoa yake ya pili ya Mkewe kipenzi Hadhrat Nusrat Jehan Begum[ra] ilikuwa na matukio mengi ya dhihirisho la mapenzi na kujaliana, ilitokea kwamba kwa sababu Mkewe alikuwa ni kutoka mjini, tena Delh na alimleta kuishi naye katika Qadian basi mwanzoni tu aligundua kwamba mkewe hawezi kulala bila taa, Naye Hadhrat Ahmad[as] alichokifanya ni aliweka taa nyumba nzima na kumfanya mkewe awe huru na mwenye furaha.
Vijana tungefuata mifano hiyo ya kuwasoma na kuwajali wenzi wetu katika hatua au siku za kwanza za ndoa zetu na kuacha kuwaza na kutaka kupewa na kufaidi raha za ndoa basi tunge onja pepo Duniani.
Mara nyingine siku hizi za mwanzo wa ndoa ndio muda wa kumuaminisha mwenzi wako kuwa hajakosea kuingia katika ndoa na wewe yaani kutengeneza mapenzi naye, na pia kikubwa ni kuzalisha na kujenga hisia za kweli kwa ajili yake.
Kitu ambacho wana ndoa wengi tunakikosa kwa wenzi wetu ni hisia za kweli, kwa sababu hisia ndizo zitakupa maumivu ikiwa mwenzi wako ana maumivu, na zitakupa nyemi ikiwa unamridhisha mwenzi wako.
Kitu ambacho inabidi tukitambue ni kwamba kabla ya mahusiano na kuingia katika ndoa kila mmoja amepata malezi na amezoea kuishi kwa namna Fulani usiyoijua kwa kipindi chote hicho, hivyo basi ina hitaji weledi na uvumilivu kupandikiza kitu kipya kwa mwenzi wako, iwe ni upendo, heshima, nidhamu na hata hisia, tunapokosea ni kwamba wengi hudhani kwamba kama amenioa au nimekuoa basi analazimika kunipenda kunisheshimu na kuwa na hisia na Mimi.
Inasimuliwa kuwa usiku mmoja mke wa Sayidna Ahmad[as] alienda kuchota maji katika kisima cha jirani na wakiwa wanapiga stori za kawaida basi alicheka kwa sauti, Mama mwenye kisima ambaye alikuwa ni mke wa mwanaye wa kambo akasema kwa kuchukizwa kuwa kama tabia ndio hiyo ya kupiga kelele kwa watu basi msije kabsa, maneno haya aliyasikia Saydna Ahmad[as] moja kwa moja, na muda huo huo aliamuru kisima kichimbwe katika nyumba yake ambacho alikisimamia na kukikamilisha ndani ya siku zisizozidi saba, akampatia mkewe kipenzi kisima chake binafsi na kumuokoa na vichambo na tambo za majirani.
Hizo ndio hisia ambazo zinatakiwa kutiririka baina ya wapenzi wawili kwani mtu anapokuwa na hisia za kweli kwa mweziwe hawezi akaruhusu mtu mwingine yeyote kuwa hata kwenye fikira zake wala hawezi kujaribu kuridhisha hisia zake kupitia mtu mwingine hata kwa kuchepuka.
Na pia suala lingine ambalo linatusumbua ni hili kwamba kumekuwa na maanguko ya kutokulinda mwenzi wetu pale wanaponyoshewa vidole au kusemwa hata wakati mwingine mbele zetu, hivi utavumiliaje kama mtu aje amseme mpenzi wako mbele zako, au ukaruhusu mtu aje aongee na mpenzi wako vyovyote atakavyo? Hio inakuwaje na sielewi inawezekanaje? Kinachotakiwa iwe ni mama au baba au yeyote wa familia au rafiki kama analolote na mwenzi wangu anatakiwa aongee na Mimi kwanza kisha Mimi ndio nitafikisha kwa mwenzi wangu, na yeyote atakaye ongea Vibaya mbele yangu kuhusu mwenzi wangu sitamuonyesha ushirikiano kwa sababu Mimi namjua zaidi au napaswa kumjua zaidi kuliko yeyote yule na kama ni la kujenga, basi nitamfikishia mwenzi wangu kama halina maana basi nitalichuja mwenyewe.
Hii inaweza kuondoa matatizo ukweni kwani mara nyingi wengi wetu wakati wa kujitafuta kimaisha huanza kuishi kwa wazazi, hivyo mara nyingi hitilafu kati na mama mzazi na mkwewe hupelekea ndoa nyingi changa nia za kuungana kwao kupotelea hewani
Hayo yote hujengwa wakati wa fungate ya ndoa au kipindi mto wa asali unatiririka na ukiweza kuyajenga hayo basi asali haitokauka mtoni.

Ujana wa Ndoa

Hiki ni kipindi kinachofuatia baada tu ya utoto wa ndoa, ni kipindi ambacho kila mmoja miongoni mwa wanandoa anakuwa tayari ameshamtambua mwenzake katika shaksia yake kwa maana ya jinsi anavyoangalia mambo, jinsi anavyofikiri, mitazamo yake, mielekeo yake na matarajio yake.
Omba Mungu kwamba kipindi hiki kikukute upo na malengo chanya kwamba kama mwenza wangu ana madhaifu nitajaribu kuyafanyia kazi na kumtengeneza kuwa yule mwenzi wa ndoto zangu.
Hapa ndipo kama uliyajenga vyema utaanza kuyafaidi matunda yako na kama hujayajenga basi cheche zake huanza kuja. Mke au Mume katika kipindi hiki habaki tu kuwa mwenza bali rafiki na mtu wa karibu zaidi na anayekujua na unaye mjua vyema. Kipindi hiki inabidi mwenza ajue machaguo yako nawe ujue yake, ifikie kiasi hiki kwamba akiona picha ya mtu wa namna fulani ajue hiyo sio mtu wa aina yako. Muweze kupiga stori ya namna yoyote na yeye aweze kukuweka bayana kuwa hujapendeza, au humridhishi kwenye mambo fulani yaani kusiwe na hofu ya kwamba sijaaga, sijapiga simu, hofu zote za makasiriko ziishe kubaki mapenzi ya dhati na maelewano ya ndani na ukweli wa wazi kabisa.

Uzee wa Ndoa

Kipindi hiki ni kipindi ambacho wanandoa wanakuwa tayari wameshaingia katika majukumu ya kulea kwa kupata matunda ya ndoa yao ambayo ni mtoto au watoto.

Kuchokana kwa wanandoa ni tatizo ambalo linatokea kwa familia nyingi, na kusababisha migogoro mingi na hata kufikia familia kuvunjika au kuishi kwa ajili tu ya kulea watoto na si vinginevyo.

Utakuta katika baadhi ya familia, Baba na Mama wanaishi katika nyumba moja, ukiwaona utadhani ni mume na mke wanaopendana, kumbe wanaishi kwa ajili tu ya kuwalea watoto wao au kwa kuogopa maneno ya watu, hali hii ni hali ya talaka ya kimapenzi *(emotional Divorce)* na ni hali mbaya, ambayo mara nyingi humpa msukumo mwanamume wa kuoa mke wa pili katika harakati za kutafuta utulivu na sehemu ya kukimbilia, au kuzaa hali za uchepukaji.

Tatizo hili la kuchokana kwa wanandoa linasababishwa na wanandoa wote wawili kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya haki za mume na mke, na pia kujua kwamba majukumu yapo lakini kila mtu bado ana nafasi kwa mwenziwe tena hio nafasi haipungui kwa sababu kuna jambo au jukumu fulani, inabidi waweze kuweka shida chini na kutupa mikono juu, inabidi waweze kujitambua kuwa wao ni viburudisho vya wao kwa wao, na kubwa ni hili kwamba kila wakuapo basi wanapozidi kukupata uzoefu mpya wa raha na ladha ya ndoa, basi inabidi wajipange kifikra kupata raha hizo katika kila hatua kwa pamoja.

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

Ishara za ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa[as]

Kutoka Uk wa 1..

na kusema wakati imani itafika mbali kama Kilimia, itarudishwa na mtu wa asili ya Kiajemi. Mtu huyo hakuwa mwingine ila Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) ambaye kwa hakika alikuwa wa asili ya Kiajemi.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) zaidi alimnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba aya hiyo 'Na kwa wengine miongoni mwao walio bado kuungana nao' kwa hakika inaunga mkono Jumuiya ya Masihi Aliyeahidiwa (as). Kama vile Maswahaba wa Mtukufu Mtume (saw) walivyoona ishara na miujiza na utimilifu wa bishara, ndivyo watu wa siku za mwisho watakavyokuwa wakishuhudia mambo kama hayo. Hivi ndivyo ilivyotokea na miaka 1,300 baada ya Mtukufu Mtume (saw), mlango huo ulifunguliwa tena na ishara kama vile kupatwa kwa mwezi na jua katika mwezi wa Ramadhani kwa mujibu wa bishara zenyewe zikatokea. Huu kimsingi ulikuwa ni muujiza wa Mtukufu Mtume (saw) ambao alitabiri kutokea kama njia ya kuthibitisha ukweli wa Mahdi wake. Hakika dalili hizi zilikuja pale alipokuwepo mwenye kudai kuwa ni Mahdi. Kuna wingi wa ishara kwa mujibu wa bishara za Mtukufu Mtume (saw), kama vile Dhus Sineen (kijinga - nyota kubwa ikimbiayo kwa kasi angani), tauni na nyingine nyingi.

Jumuiya ya Waumini wanaofanana na Maswahaba wa Mtukufu Mtume (saw).

Khalifa mtukufu (atba) alizidi kumnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba hakuna Jumuiya nyingine ambayo ina mfanano na Maswahaba wa Mtukufu Mtume (saw). Ishara walizozishuhudia Maswahaba leo zinashuhudiwa; dhiki na matatizo waliyokumbana nayo Maswahaba, wanakabiliana nayo leo; Ishara za Mwenyezi Mungu zilizo wazi ambazo Maswahaba waliziona na hivyo kuwatia nguvu imani, zinaonekana leo; kama vile Maswahaba walivyolia katika sala na kuona dalili na ndoto, zinaonekana leo; kama vile Maswahaba walivyotoa mali zao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu, ndivyo watu wanavyofanya leo. Kama vile Maswahaba hawakuogopa kifo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, walikuwa na mioyo nyororo, na wakatembea juu ya njia ya haki, vivyo hivyo ndivyo ilivyo leo kwa watu wa Jumuiya hii. Hivyo basi, sifa zote hizo ambazo zilipatikana katika Maswahaba zinaonekana kuwa zinaakisiwa ndani ya Jumuiya ya Masihi Aliyeahidiwa (as).

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) aliendelea kumnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba Masihi wa siku za mwisho (as) angebeba mifanano miwili; kufanana na Isa / Yesu (as) kwa sababu yake angeitwa Masihi, na kufanana na Mtukufu Mtume (saw) kwa ajili yake angeitwa Mahdi. Ujio wa Isa (as) ulikuja wakati Taurati na mafundisho yake yakiwa katika mashambulizi makali na watu wakaudhihaki utume wa Musa (as). Kwa hivyo, kwa kumtuma Isa (as) miaka 1400 baada ya Musa (as), Mwenyezi Mungu alikusudia kutia nguvu tena kipindi cha Musa na kutoa ishara mpya kwa ukweli wake. Kuja kwa Masihi Aliyeahidiwa (as) kulikuwa kwa namna ile ile, kwa sababu zilezile; kuulinda Uislamu dhidi ya maelfu ya mashambulizi yanayofanywa dhidi yake, Mtukufu Mtume (saw) na Qur'ani Tukufu kwa ishara na dalili mpya. Ilikuwa hivyo kwamba Masihi Aliyeahidiwa (as) aliagizwa na Mungu kutangaza kwamba alikuwa ametumwa na Mwenyezi Mungu.

Hitajio Kubwa la Mwongozo wa Kimungu

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alizidi kumnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema, wengine wanasema kwamba Isa (as) alikuja kuhuisha ujumbe wa Musa (as) kama nabii. Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema kwamba mlango wa kuja Mtume mwingine wa kuleta sheria baada ya Mtukufu Mtume (saw) umefungwa, kama ilivyothibitishwa kupitia Qur'ani Tukufu na maneno ya Mtukufu Mtume (saw). Hata hivyo, hii haimaanishi kwamba mlango wa kuzungumza na kuunganishwa na Mungu umefungwa. Kwa hiyo, pamoja na kuthibitishwa kwamba Isa (as) alikufa, ilikuwa hakika kwamba Masihi lazima adhihirike duniani, na kwa mujibu wa bishara za Mtukufu Mtume (saw) na kwa kuzingatia hali ya Waislamu ilikuwa ni hakika kwamba mtu mmoja alipaswa kutumwa na Mungu ili kuhuisha ujumbe wa Uislamu. Kwa hivyo, inapaswa kukubalika angalau kwamba hata Walii (rafiki) wa Mwenyezi Mungu anaweza kutumwa na Mungu kwa kazi hii. Zaidi ya hayo, inathibitishwa kupitia Hadithi kwamba hata Muhaddathin wamejumuishwa miongoni mwa wale waliotumwa na Mungu, kama vile Mitume walivyokuwa. Hata zaidi kwa hili, inathibitishwa kupitia Hadithi kwamba Masihi angekuwa nabii. Hata neno 'Mtume' lililotumika katika mstari wa 3 wa sura ya 62 pia linamrejelea Masihi Aliyeahidiwa (as). Huu kimsingi ni uthibitisho zaidi wa kimo na ukweli wa Mtukufu Mtume (saw).

Mungu Anamtuma Mujaddid Katika mzunguko wa kila Karne

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) aliendelea kumnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba alipoona hali ya sasa ya ulimwengu, Mungu alimtuma Masihi Aliyeahidiwa (as) ili kueneza ukweli. Ilikuwa hivyo kwamba Masihi Aliyeahidiwa (as) alitangaza waziwazi kwamba yule ambaye angetumwa mwanzoni mwa karne ili kuuvuta ulimwengu kuelekea kwenye matengenezo hakika alikuwa yeye. Ilibainishwa kwake kupitia ufunuo wa Mwenyezi Mungu kwamba Masihi Aliyeahidiwa kuja na Mahdi ambaye angehuisha imani kwa ishara mpya ambazo zilibashiriwa miaka 1,300 kabla na Mtukufu Mtume (saw) hawakuwa wengine ila yeye, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as).

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alizidi kumnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba wakati ulimwengu ulipokuwa ukienda mbali na Mwenyezi Mungu na kugeuka zaidi na zaidi kuelekea ukafiri, heshima ya Mwenyezi Mungu inaelekeza kuwa Nafsi Yake inapaswa kudhihirika kwa ulimwengu kwa mara nyingine tena. na ilikuwa ni kwa sababu hii na kuonyesha dalili za wazi kwamba Masihi Aliyeahidiwa (as) alitumwa duniani kwa wakati huu na katika zama hizi.

Kwa nini Madai ya Masihi Aliyeahidiwa (as) Lazima Yakubaliwe

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) kisha akamnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye aliwajibu wale waliohoji ni vipi wangeweza kujua kwamba yeye kweli alikuwa Masihi Aliyeahidiwa (as). Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema kwamba dalili na ishara zote zilizokuwa ziambatane na ujio wa Masihi Aliyeahidiwa (as) zimetimizwa ndani yake, wakati wake na nchi yake.

Kwa hiyo, ishara kama vile kupatwa kwa jua, tauni, matetemeko ya ardhi na nyinginezo zisizohesabika zote ni dalili zinazoonyesha wazi kuwa sio tu kwamba huu ulikuwa wakati wa ujio wa Masihi wa siku za mwisho, bali kwa hakika yeye alikuwa ndiye Masihi Aliyeahidiwa.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) aliendelea kumnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba kulikuwa na ishara mbalimbali za kiakili ambazo pia ziliambatana na ujio wake. Kwa mfano, Mhindu mmoja alitaka kuuandaa kongamano la dini mbalimbali zilizopo duniani na akamwendea Masihi Aliyeahidiwa (as) ili kuandika hotuba kuhusu Uislamu. Alijibu kwamba hawezi kusema chochote bila kuongozwa na Mungu. Kwa hiyo, Masihi Aliyeahidiwa (as) aliomba kwa ajili ya kupatiwa uwezo wa kuandika makala ambayo ingezishinda nyingine yote. Kisha akaona kwamba uwezo wa mbinguni wa kuandika hotuba hii uliingizwa ndani yake, na kisha akaandika kwa kasi sana kiasi kwamba wale wanaonakili hawakuweza kuendana na kasi yake. Mara tu alipomaliza kuandika, Mungu alimfunulia kwamba hotuba hiyo ingeshinda hotuba zote. Kwa hiyo, mara tu hotuba hii ilipotolewa, msimamizi alitangaza mbele ya watu wote kwamba hakukuwa na shaka kwamba hotuba hiyo ndiyo ilikuwa bora zaidi katika mkutano huo. Machapisho mengi pia yalithibitisha waziwazi ubora wa makala haya na kuwa bora zaidi katika mkutano huo. Hii bila shaka ilikuwa ni hotuba iliyojulikana kama Hekima ya Mafundisho ya Islam.

Kukubalika kwa Maombi ya Masihi Aliyeahidiwa (as).

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alizidi kumnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba Mungu alimfunulia kwamba ufasaha utatiririka kutoka kwenye midomo yake. Kupitia maandishi yake ya kina, watu wa imani na asili tofauti wamelazimika kuthibitisha kwamba maandishi yake hayana mlingano, iwe katika Kiurdu au hata kwa Kiarabu.

Kisha zikawa pia dalili za kukubaliwa kwa maombi. Wakati mvulana mmoja aliumwa na mbwa mwenye kichaa na ikaamuliwa kwamba hakuna kitu kingine chochote ambacho kingeweza kufanywa kwa ajili yake na angekufa hivi karibuni, Masihi Aliyeahidiwa (as) aliomba sana na kwa maumivu makali kwa ajili yake. Hali maalum ya kukubaliwa ilidhihirika kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. na maombi yake yakaleta mabadililo ya kimuujiza kwa kijana yule na ndani ya siku chache akapona kabisa. Ndipo ikawa wazi kwamba ugonjwa huu ndani ya mvulana haukukusudiwa kumfanya aangamie, bali ilikuwa ni fursa ya ukuu wa Mungu kudhihirika kwa mara nyingine tena.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alimnukuu zaidi Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alitaja ishara ya Dk. Alexander Dowie, ambaye aliangamia baada ya kufanya Mubahala (dua ya maombi) dhidi ya Masihi Aliyeahidiwa (as). Mtu ambaye alikuwa na sifa kubwa na uwezo aliangamia kwa fedheha kama matokeo ya kumkanusha kwake Masihi Aliyeahidiwa (as) na kumpa changamoto kwenye tambio la maombi.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alizidi kumnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye aliwajibu wale wanaosema kwamba Mungu apishe mbali kuwa yeye ni mwongo na ana ndani yake wingi wa makosa na maovu. Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema kwamba kama hili lingekuwa kweli, basi itakuwaje kwamba Jamaat yake iendelee kufanikiwa na Mungu anaendelea kuonesha dalili za wazi kwa niaba yake. Je, hili halithibitishi ukweli wake kwa uwazi?

Masihi wa Kuunganisha Umma wa Kiislamu

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba lau wapinzani wangesoma vitabu vyake na kutafakari juu ya ishara za kiungu zilizoambatana na Masihi Aliyeahidiwa (as). Wapinzani angalau wanakubali kwamba zama za sasa zinataka ujio wa mrekebishaji na Mahdi, lakini wanamkanusha yule ambaye amekwisha kuja, na wakati huo huo wanaupoteza umma wa Kiislamu. Ishara za mbinguni ziliambatana na ujio wa Masihi Aliyeahidiwa (as), lakini watu hawa bado hawazitambui. Iwapo Waislamu leo wangemtambua na kumkubali Masihi Aliyeahidiwa (as), basi Umma wa Kiislamu unaweza kupata ubora duniani; la sivyo basi hali yao itabaki kama ilivyo. Mwenyezi Mungu awape akili na uelewa.

Khalifa mtukufu (atba) amesema kuwa katika mwezi wa Ramadhani pamoja na kujiombea nafsi zao na Jumuiya, Waahmadiyya pia wanapaswa kuuombea Umma wa Kiislamu, Mwenyezi Mungu awafumbue macho, awatoe gizani, na awawezeshe kutambua hilo. Masihi Aliyeahidiwa (as) na Jumuiya yake ndio wanaoelewa kwa hakika hadhi ya Mtukufu Mtume (saw) kama Khaatamun Nabiyyiin (Muhuri wa Manabii).

Maombi kwa Waahmadiyya Kote Ulimwenguni

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) aliwataka wanajamaat kuwaombea Waahmadiyya wa Pakistan na nchi ya Pakistani yenyewe; Mwenyezi Mungu ainusuru nchi na wale wanaotaka kuleta fujo na viongozi wanaojitumikia wenyewe. Khalifa mtukufu (atba) pia alihimiza maombi kwa Waahmadiyya huko Burkina Faso na Bangladesh. Khalifa mtukufu (atba) aliwaombea Waahmadiyya wote duniani wabaki salama na kila madhara, Mwenyezi Mungu awajaalie Waahmadiyya uthabiti na awazidishie imani.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) pia alihimiza maombi kwa ajili ya ulimwengu kuokolewa na maangamizo. Hali za ulimwengu leo zinaufanya kusimama kwenye kilima cha moto. Ulimwengu hausimami tu ukingoni mwa uharibifu wa kimwili kwa namna ya vita, bali pia uharibifu wa kimaadili unaoendelea kuongezeka kadiri watu wanavyomwacha Mwenyezi Mungu; warekebishe njia zao, wasije wakavuta ghadhabu ya Mwenyezi Mungu.

Khalifa mtukufu (atba) alimuomba Mwenyezi Mungu awalinde Waahmadiyya na maovu yote na awawezeshe kutekeleza wajibu na wajibu wao huku akiwaweka katika

...Mwisho

Maulamaa Wawili

Na.
Mahmood Hamsin Mubiru
Kiwalani Dar es Salaam

Maulamaa hawa wawili Sheikh Muhammad Munawwar na Sheikh Jamil Rahman Rafiq walipenda na



kuheshimu lugha ya Kiarabu. Mapenzi yao yalitokana na maelezo ya ufafanuzi aliotoa Masih Aliyeahidiwa Hazrat Ghulam Ahmad[as] kuhusu Kiarabu katika Kitabu chake *Minal Rahman.* Ambamo amejenga hoja kuwa Kiarabu ni mama wa lugha zote. Kwa sababu kutumwa Masih Aliyeahidiwa Hazrat Ghulam Ahmad[as] shabaha yake ilikuwa ni kuonesha ubora na shani ya Islamu ukilinganisha na Dini nyingine, Masih Aliyeahidiwa Hazrat Ghulam Ahmad[as] hakuacha mwanya wowote wa kudhihirisha hilo, ndio sababu ya kuandika Kitabu hicho. Aliandika Kitabu hicho kati ya Aprili na Mei 1895, ambacho ni Bahari pana ya utafiti wa Kisayansi na ukweli huo *Inshallah* unaendelea kudhihirika sawa na siku zinavyokwenda. Katika Kitabu hiki anathibitisha kuwa Kiarabu ni mama wa lugha zote. Hivyo ni lugha yenye sifa ya kufikisha ujumbe wa mwisho wa Allah uliokamilika kwa binadamu wote.

Katika Kitabu hiki Masih Aliyeahidiwa[as] anajadili mambo matatu:-

1. Kuna kitu kinachounganisha lugha zote Duniani.
2. Kiarabu ni mama wa lugha zote.
3. Kwa sababu ni lugha iliyokamilika.

Kiarabu ni lugha ya Wahyi kuonesha kuwa kuna kitu kinachounganisha lugha zote. Maulvi Nurud-Din[ra], Abdul Karim na Munshi Ghulam Qadir Fasih[ra] Kh Kamal-u-Din Mirza Khuda Bakh, Sheikh Mufil Muhammad Sahib, Miyan Muhammad Khan, Munshi Ghulam Muhammad Nawili hawa ndio waliofanya kazi kubwa. Kwa kutumwa na Masih Aliyeahidiwa[as]

Ili kuonesha kuwa Kiarabu ndio chimbuko ya lugha zote. Masih Aliyeahidiwa[as] anasema ya kwamba, Kiarabu ni lugha ya asili ya maumbile. Na ina uwezo wa kueleza na kutafakari kuhusu uzuri wa maumbile.

Kiarabu kina sifa zinazopatikana katika lugha zote. Kiarabu kina misamiati iliyokamilika, mizizi ya maneno yanayofafanua maana za ndani za neno. Mada yoyote iwayo inaweza kuelezwa kwa kutumia Kiarabu na hakuna usichowezi kuelewa unapozama kwenye mizizi. Kuna mpangilio maalumu uliomo katika lugha na mpangilio huo una uhusiano. Wakati lugha nyingine zinaeleza jambo kwa kutumia maneno mengi. Kiarabu kina uwezo wa kueleza neno moja tu na likawa linatosheleza. Hisia za ndani zinaweza kuelezwa kwa ubingwa wa hali ya juu kutumia lugha hii.

Masih Aliyeahidiwa[as] alitangaza kuwa angeliweza kutoa rupia 5000. Kwa yeyote anayeweza kuonesha lugha iliyobora kuliko Kiarabu. Kuonesha utajiri, uzuri na kuwa lugha ya Dunia, Masih Aliyeahidiwa[as] aliandika Kitabu hiki. Minal Rahman.

Ni sababu hizo zilizowafanya wanazuoni hawa wawili wajifunze kwa bidi lugha hii adhimu. Sheikh Muhammad Munawwar Sahib mtihani wake wa mwisho wa Shahada katika jimbo zima la Punjab, kupitia Chuo Kikuu cha Punjab, yeye alisimama wa kwanza katika Shahada ya H.A**(Honours in Arabic)**. Hii zawadi kubwa aliyopewa na Allah, hakupenda kuifaidi yeye pekeyake. Alifanya kila juhudi kuwafundisha na wengine. Kila mara baada ya Magharib Waahmadiyya na wasio Waahmadiyya walikusanyika mbele ya Masjid Salaam ambapo Darasa la Kiarabu liliendeshwa. Tuliokuwa pembeni tulifaidi matamshi yake mazuri ya Kiarabu na yale mashairi yaliyokuwa yanasomwa na wanafunzi wake. Wanafunzi ambao hawakukosa katika Darasa hilo ni pamoja na Rashid Msabaha (ambaye licha ya Kiarabu alijifunza na Kiurdu), Nyumba Mussa, Muhammad Said Kibindu, Muhamedi Said (Kivukoni), Mbwana Mgunda na Sultan Ungando. Sheikh Jamil Rahman Rafiq Sahib naye alikuwa na bidii kubwa ya kufundisha. Kwa hakika alifurahia kazi hii na uliweza kuiona bashasha aliyokuwa nayo ya kuwapatia watu elimu. Miongoni mwa wanafunzi wake ni pamoja na Nyumba Mussa, Mohamedi Saidi(Kivukoni), Muhammad Saidi Kibindu, Hanif Mpogo na Sultan Ungando.



Wapinzani wa Jumuiya ya Ahmadiyya walitumia hoja Waahmadiyya kutojua Kiarabu. Maulamaa hawa wawili walivunja hoja kwa kuwaambia wapinzani kuwa, kujua Kiarabu bila kumfuata Nabii wa Allah ni kazi bure. Waliwauliza wapinzani ni kwa kiasi gani Kiarabu kilimsaidia Abuu Jahl kufahamu ukweli wa Mtukufu Mtume Muhammad[saw]. Nani aliyekuwa bora, yule aliyefahamu Kiarabu, matawi na shina lake au yule hata kutamka hakuweza na katika Adhana yake akawa anasema Asahadu, na Mtukufu Mtume[saw] akasema kuwa Adhana hiyo ilikuwa inakubalika mbinguni.

Sifa ya Sayyidna Bilal haikuwa Kiarabu bali Taqwa na Ushahidi huo anautoa Mtukufu Mtume[saw] katika safari yake ya Miraji. Alipokuwa akienda huku akiongozwa na Sayyidna Jibril[as]. Kila akipiga hatua anasikia mtu mbele yake akitembea. Alitaka kuuliza mtu mbele yangu akitembea, kuna nani mbele yangu aliyetangulia? Akajibiwa huyo ni Sayyidna Bilal. Akawa anauliza kitu gani unafanya?

Mimi naanza asubuhi natunza udhu wangu nabaki nao mpaka Adhuhur. Hata nikisha Kwenda haja, nitatawaza na kusali rakaa mbili na kuendelea na udhu wangu.

Wapinzani waliokuja na kimbelembele cha dhana ya kuwa Waahmadiyya hawajui Kiarabu, walipata kuzaliwa vijana waliotoka Saudia na mbwembwe nyingi za Kiarabu. Walielezwa kuwachokoza Waahmadiyya katika Kiarabu. Bwana mmoja ambaye jina lake tunalifupisha na kumuita S.J.M alibisha hodi na sisi aliotukuta mlangoni alianza kutumiminia Kiarabu bila kutaka kutamka hata neno moja la Kiswahili. Sisi tulimuelekeza ofisini ili apambane na Mwaarabu Mwenzie. Nilimsindikiza hadi kwa Sheikh Muhammad Munawwar Sahib. Kijana huyo wa Rufiji aliendelea kumimina Kiarabu wakati Sheikh Muhammad Munawwar Sahib anaandika. Alimaliza kwa Kiarabu akamwambia kuna makosa makubwa kumi ya Kiarabu umefanya. Akaanza kumueleza kijana huyo kutoka Rufiji akaanza kuhema asiwe na lolote la kujitetea, ndipo Sheikh Munawwar Sahib alipomueleza kuwa ni vizuri kuzungumza lugha uliyofunzwa na mama kuliko kuparamia lugha ambazo unazijua kwa mashaka. Kijana huyo kwa aibu tulimsindikiza huku sisi akina Yakhe tusiojua hata maneno wawili ya Kiarabu tukimuambia arudi Saudia kunyoosha Kiarabu chake!!

Bustani ya Washairi

FUNGA SWAUMU NI DAWA
Baada siku kalili, toka sasa navyojuwa
Ule mwezi wa fadhili, na utukufu ukiwa
Inshaallah utawasili, basi tujiweke sawa
Funga Swaumu ni dawa, ya maradhi mbalimbali.

Ni amri ya Jalali, Yule wa kuabudiwa
Nalo funzo la azali, nasi tumeagiziwa
Kwa hivyo halipo swali, tekelezo latakiwa
Funga Swaumu ni dawa, ya maradhi mbalimbali.

Una salama ya mwili, huugui upo powa
Ramadhani kula hali, uifunge kwa taqwa
Haipotezi amali, bali thawabu tapewa
Funga Swaumu ni dawa, ya maradhi mbalimbali.

Viungo vyetu dhalili, magonjwa tele yauwa
"UWONGO" wa sampuli, wasema na kusemewa
Ndimi zetu hazikuli, kauli njema na sawa
Funga Swaumu ni dawa, ya maradhi mbalimbali.

"UAMINIFU" akali, kila nyumba wapunguwa
Waume na wanawali, wageni hadi wazawa
Na mno juu ya mali, wachache sana watawa
Funga Swaumu ni dawa, ya maradhi mbalimbali.

"KUSINGIZIA" ajali, kibaya unachopewa.
Kinavuruga miili, ya wale wasingiziwa
Wasingizia hawali, bali moto watapewa
Funga Swaumu ni dawa, ya maradhi mbalimbali.

"USENGENYI" ni singeli, wacheza wamenogewa
Waambukiza salali, haraka si kuchelewa
Unaharibu amali, ya watu wema watawa
Funga Swaumu ni dawa, ya maradhi mbalimbali.

UZABIZABINA" hali, wadhoofisha utawa
"UMBEYA" kisulisuli, unasi wasusuliwa
Salama bwana kuswali, na kufunga tungejuwa!
Funga Swaumu ni dawa, ya maradhi mbalimbali.

"MASINGIZIO" katili, yauwa na kuuawa
Ni mwendo wa kijahili, si mwendo wa sawa sawa
Ukiwa nao badili, Allah atakuokowa
Funga Swaumu ni dawa, ya maradhi mbalimbali.

"SHUKU" ina idhilali, wala haina satuwa
Inaumiza akili, na wasiwasi kutiwa
Ghafla hufa manzili, wana wakawa wakiwa!
Funga Swaumu ni dawa, ya maradhi mbalimbali.

Haya maradhi makali, mengine sikutongowa
Tiba yanastahili, dini iwe yaokowa
Twenende hospitali, weye nami twangojewa
Funga Swaumu ni dawa, ya maradhi mbalimbali.

Tupate dozi kamilli, na afuwa tutapewa
Nyoyo zitakuwa tuli. Zile za kurehimiwa
Zitazobeba shughuli, ile ya kuokolewa
Funga Swaumu ni dawa, ya maradhi mbalimbali.

Tamati shairi hili, Ramadhani imetuwa
Asharul fadhili, nyingi zisohesabiwa
Ya Allah dhuljalali, funga iwe barikiwa
Funga Swaumu ni dawa, ya maradhi mbalimbali.

Al- Ustadh Mhenga
Khamisi S.S. Wamwera
Kimbangulile - Mbagala Rangitatu

Mtema Kuni
Kisa cha mtema Kuni, nipe nipate faidi
Nikielewe kiini, ipanuke yangu fuadi
Ilikuwa msituni, au ni huku biladi
Nipe kisan a mkasa, kisa cha mtema kumi.

Mahmoud Hamsin Mubiru (Wamamba)
Migombani-Kiwalani.

USHOGA
Ninakuomba Rabuka, tujalie mwisho mwema
Tumeshaparaganyika, kama tayari kiama
Ushoga wanautaka, kila hali kwa lazima
Rabbi taqabbal Dua, tuepushe na kikombe

Mashoga wapaparika, na kunema wananema
Viuno wamevunjika, hawapandishi milima
Waweza kudhani Kaka, kumbe Jitu sio zima
Rabbi taqabbal Dua, tuepushe na kikombe

Miraba imekatika, Jitu kubwa zima zima
Hicho kisauti kaka, mbona wakosa heshima?
Hajali hana mipaka, na kunema ananema
Rabbi taqabbal Dua, tuepushe na kikombe

Wazungu wana vibweka, kuulazimisha uma
Eti haki wanataka, misuli imetumbama
Mashoga kutambulika, duniani kwa lazima
Rabbi taqabbal Dua, tuepushe na kikombe

Nawasihi nyi wakaka, msiupotoshe uma
Kwanza muwe na mipaka, jamii iwe salama
Muache kucheka cheka, nyakati muweze soma
Rabbi taqabbal Dua, tuepushe na kikombe

Na ndoa mnaoleka, hamuogopi kiama
Hivi jamani wakaka, mmeshindwa kujituma?
Kusanyeni hata taka, ila sio kupindama
Rabbi taqabbal Dua, tuepushe na kikombe

Kwanza nimeshagutuka, wengi wao si vilema
Wamezaliwa Mashoka, na kupima wanapima
Ila wanabadilika, kuiga ya kina mama
Rabbi taqabbal Dua, tuepushe na kikombe

Ila wanabadilika, kuiga ya kina mama
Mara mekapu jipaka, na sauti ya kimama
Mara waanza kunyuka, viwalo vya kinamama
Rabbi taqabbal Dua, tuepushe na kikombe

Kuiga visoigika, unapukutika uma
Mara jana mlitoka, mkanywa pombe na nyama
Ni mzuri yule Kaka, macho kama ana uma
Rabbi taqabbal Dua, tuepushe na kikombe

Kutwa unajichomeka, kwa wadada majimama
Miguu 'metambalika, katikati ya wamama
Kutwa unacheka cheka, unashinda siku nzima
Rabbi taqabbal Dua, tuepushe na kikombe

Mungu anakasirika, tabia za usodoma
Wataka kutambulika, ufahamike na uma
Unapaswa kuongoka, kuunusurisha uma
Rabbi taqabbal Dua, tuepushe na kikombe

Wazungu 'metajirika, 'mepata hela mapema
Afrika bado vibweka, wao watupa uzima
Na tumeshashawishika, 'mewakabidhi mtima
Rabbi taqabbal Dua, tuepushe na kikombe

Na muache kushoboka, na msiwe hima hima
Nje ya nchi kutoka, ughaibuni kusoma
Fata lilo kupeleka, 'siufatishe mtima
Rabbi taqabbal Dua, tuepushe na kikombe

Ni Tanzania kumbuka, 'nchi mejawa heshima
Usije kukurupuka, kwa halaiki kusema
Mashoga mwaburudika, bakora tutakuzima
Rabbi taqabbal Dua, tuepushe na kikombe

Muda umetamatika, napumzika mapema
Kesho niweze andika, ili mpate kusoma
Mpate kuburudika, tukijaliwa uzima
Ushoga ni marufuku, twajiepusha na lana

Abdallah Kalindima
#CHUMACHAKAVU
Kalindimasenior@gmail.com

Hodi Nijile Dodoma
Hasani nabisha hodi, Mlangoni nasimama
Kwenu mafundi Stadi, washairi wa heshima
Zifungueni fuadi, mnipokee Ghulama
Hodi nijile Dodoma, Hasani nabisha hodi.

Jitukali Mahamudu, mjukuu muadhama
Sifazo nzuri Zaidi, sitasita kuzisema
Kuja uliko ni Idi, nafurahika mtima.
Hassan R. Hassan - Idara ya Kiswahili
Chuo Kikuu cha Dodoma

Karibu Dodoma
Tawile bingwa mweledi,karibu kwetu Dodoma
Kukujibu sina budi, japo ni mwezi mzima
Zako tungo maridadi, beti wazipanga vyema
Karibu kwetu Dodoma, Karibu bwana Hasani.

Kawaida yetu jadi, afikapo muadhama
Si hoja kubisha hodi, aje anademadema
Nyumba itawashwa udi, na beti zitazizima
Karibu kwetu Dodoma, karibu bwana Hasani.

Vyakula vya mazidadi, sharubati za kupima
Utaandaliwa hadi, ule biliani kwa nyama
Ulale kifudifudi, na kichwa ukiegama
Karibu kwetu Dodoma, karibu bwana Hasani.

Manju katika idadi, Malenga waliozama
Waje toka Bariadi, Kagera Darisalama
Watano wasiozidi, Hasani umesimama
Karibu kwetu Dodoma, karibu bwana Hasani.

Sisi twajiona Iodi, twamshukuru Karima
Dodoma tutasaidi, busara nazo hekima
Twende tunataradadi, Masheikh na maamuma
Karibu kwetu Dodoma, karibu bwana Hasani.

Sifa tunatabaradi, namshukuru Rahima
Malenga nisohasidi, kitungo sijachechema
Zangu tungo ni shadidi, ningali ninanguruma.
Karibu kwetu Dodoma, karibu bwana Hasani.
Hamdoany Zahran Mansour
Dodoma.

Dunia
Dunia ninapendeza, sura yangu yavutia
Maua yakupendeza, bahari zakuvutia
Milima ya kuliwaza, majengo yalotulia
Unanini we akhera, Dunia lichonishinda?

Akhera
Mimi siwezi jisifu, kwani mungu kakwambia
Nguvu soda wajisifu, unamwisho we dunia
Mbwembwe zako zinakifu, daima utapotea
Utaniacha akhera, mbali utapotelea.

Dunia
Hilo walijua weye, viumbe wajatambua
Raha zangu kumbatiye, kesho kutofikiria
Mimi ndiye nipendwaye,sitarehe nazitoa
Unanini we akhera, Dunia lichonishinda.

Akhera
Wajinga wako Dunia, welevu wangu akhera
Akili wenye tumia, peponi wenye kung'ara
Dunia wewe ni njia, mafikio ni akhera
Unanini we dunia, paka Mimi koromea

Dunia
Uyasemayo ni kweli, urembo nimejaliwa
Kasoro yangu asili,umuri napungukiwa
Mi shamba la kulimia, zao kwako kuletewa
Unanini we akhera, Dunia lichonishinda

Akhera
mekushinda Kila hali, walowema metambuwa
Mito yenye asali, maziwa maji ya kunywa
Mimi mzuri asili, akili jawahi fikwa
Nitafuteni akhera, milele mufurahikwe

Mtunzi
Masihi omary stambuli kisagwa

Kumbe ni Umasikini!!

Na. Mwandishi wetu.

Mataifa ya Magharibi na vyombo vyake vya Habari, hayajaacha jiwe lolote bila kugeuzwa na tone la mwisho la wino kutumika ili kuaminisha Dunia kwamba kuzuka kwa vikundi vya ugaidi kama vile uyoga kunatokana na Islam. Chuki hii, masingizio haya, vyote hivyo havikuanza leo, vina hisitoria ndefu na ya kutia kichefuchefu.

Hasa Kalamu imetumika sana kupaka Matope Islam. Wasomi wa Magharibi walitumia uwezo wao wa hadaa kutunga hekaya zao ***Maxime Rodinson*** katika ***Mohammed,*** anauma na kupuliza lakini hatimae tunaona vizuri chuki yake dhidi ya Islam. Kwa uwazi anakataa Kuruani Tukufu. ***Hans Kung***- anasema *Martin Luther* alitaka Kuruani Tukufu itafsiriwe ili watu waone (Allah apishe mbali) laana, aibu, uongo uliomo katika Kuruani! *Professor William Montogomery Watt* katika vitabu vyake ***Muhammad al Mecca, Muhammad al Madina,*** kama anavyosema *William Shakespeare*. Linaonekana ua la Walidi kumbe ndani yake kuna Nyoka! Ni nyoka watupu katika vitabu vyake.

Adui hachoki wala hapumui hadi umeangamia. Hata hivyo, mara nyingine adui anashindwa kuficha ukweli. Hivi karibuni Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo, katika taarifa yake kwa Umma, amesisitiza kuwa Ghasia, fujo zinazotokea katika bara la Afrika, chimbuko lake ni umasikini na ukosekanaji wa fursa hususani kwa vijana. Shirika hilo la Umoja wa Mataifa linasema ugaidi na vurugu vina mvuto mkubwa kwa vijana wasio soma na kutoka katika nchi zilizotengwa na Dunia na kuwa na Miundo mbinu mibovu na isiyo na tija. Vijana wengi hawana kazi na wananyanyapaliwa na walio madarakani.

TAFUTA MANENO

Tafuta majina 20 ya wanyama hapo chini kwa kuyazungushia na Penseli

M	A	J	I	N	A	Y	A	N	E	W	A	N	Y	A
M	A	F	A	R	A	S	I	B	Y	W	Q	L	V	I
N	Y	U	M	B	U	R	M	H	C	A	T	X	M	Y
T	C	N	Y	X	Z	O	H	X	R	G	N	U	X	N
G	F	A	R	U	'	K	A	P	J	X	G	I	T	Y
W	N	D	L	G	L	I	W	V	H	N	K	T	C	U
K	Y	G	N	N	M	J	K	R	A	X	U	S	M	N
T	O	F	U	A	Y	M	G	Y	Y	J	N	I	L	G
H	X	N	G	R	T	X	N	H	L	M	G	M	F	U
B	M	N	D	M	U	L	L	P	N	L	U	B	G	N
U	M	M	J	O	B	W	A	G	O	R	R	A	T	Y
I	R	N	B	I	O	W	E	M	K	P	U	C	E	U
B	J	C	U	U	B	P	U	N	D	A	O	K	M	N
U	D	H	D	M	Z	N	T	N	L	M	V	Q	B	G
I	C	N	Y	U	K	I	G	T	D	M	R	W	O	U

UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



Jinsi ya kupika Karanga za Mayai

Na **Mtandao**



MAHITAJI

1. Karanga kilo moja.
2. Mayai 3 inategemea na ukubwa.
3. Chumvi kijiko kimoja.
4. Sukari kiasi unachohitaji.
5. Unga wa ngano robo kilo(kidogo tu).
6. Mafuta ya kupikia.

JINSI YA KUANDAA

1. Chukua karanga weka katika sinia, chambua kuondoa karanga mbovu, zilizokatika na taka taka.

2. Baada ya kuchambua weka katika bakuli au chombo cha kukandia, piga mayai katika chombo pembeni na uweke chumvi.
Tia mayai katika karanga na kisha zichanganye kuhakikisha zote zimekolea mayai.

3. Chukua kiasi cha sukari unachokadiria kitakufaa Tia katika ule mchanganyiko wa karanga, mayai na chumvi kisha Changanya ili sukari inate katika karanga zote.

4. Chukua unga Tia Katika mchanganyiko wako, changanya vizuri kuhakikisha karanga zote zimekuwa nyeupe kwakufunikwa na unga.

5. Weka mafuta kiasi kwenye kikaango, yakichemka anza kukaanga karanga zako hakikisha unazitoa kabla hazijawa Brown sana usijeunguza karanga zako

NB ; kuwa makini na watoto, haukawii kukuta zimeisha!

Jamia Waadhimisha Siku ya Masihi Aliyeahidiwa as

Kutoka Uk wa 1..

wa Quran tukufu iliyosomwa na Haafidh Abdurrahman .R. Rundo na kufuatiwa na shairi la kiurdu lililosomwa kwa ustadi na Ismail Abdullatif Pembe.

Baada ya shairi hilo la kiurdu ilifuata hotuba yenye maudhui isemayo,"Maisha matakatifu ya Hadhrat Masih Mauud as kabla ya madai yake" hotuba hiyo ilitolewa na Ustaadh Salim Ngenzirabona .Mhutubu alianza hotuba kwa kunukuu aya ya Kurani Tukufu kutoka katika sura Yuunus aya yake ya 17 [10:17] kurejea
mifano na matukio mbalimbali katika maisha matakatifu ya mjumbe huyu wa
zama kabla ya madai yake ya kuwa masihi na Imam Mahdi, mifano ambayo
inathibitisha pasi na shaka ya kuwa hata kabla ya madai yake, yeye alikuwa ni mtu mwema, mkarimu na mtakatifu wa hali ya juu kabisa na hali hii inathibitisha ukweli wake.

Baada ya hotuba hiyo, ilifuata hotuba ya maudhui isemayo, "Mapenzi ya Hadhrat Masih Mau'd as kwa Mwenyezi Mungu." Hotuba hiyo ilitolewa na Maulana Shaikh Shafii Memon Sahib. Sheikh Sahib alitaja maneno na matukio kadha wa kadha ya kusisimua yanayoonyesha jinsi Hadhrat Masih Mau'ud as alivyompenda Mwenyezi Mungu na alivyojitolea kumtumikia katika maisha yake yote.

Kisha ilifuata hotuba yenye anuani isemayo, "Shauku na jazba ya Hadhrat Masih Mau'ud as katika mahubiri." Hotuba hii ilitolewa na Maulana, Shaikh Karimud-Din Shams Sahib – Shaikh wa mkoa wa Morogoro. Shaikh Sahib alianza hotuba yake kwa kusoma aya ya 163 kutoka katika Suratul An'aam (6:163). Shaikh Sahib alinukuu kauli na matukio mengi ya Hadhrat Masih Mau'ud as yanayoonyesha na kuthibitisha kuwa mbele ya mahubiri, yeye hata njaa hakuisikia. Kwa ujumla,
mzungumzaji aliwathibitishia wasikilizaji ya kuwa, maisha yote ya masihi aliyeahidiwa as yalikuwa ni mahubiri.

Baada ya hotuba hiyo, zilifuata nasaha fupi kutoka kwa mgeni rasmi(Amiir na
mbashiri Mkuu) ambaye alianza kwa kusoma aya ya 3 kutoka katika Suurati-Ssaaf (61:3) ambayo inawatahadharisha waaminio ya kuwa wasiseme wasiyoyatenda. Kisha alisema kuwa leo watu wengi wanadai kuwa ni waislamu, lakini vitendo vyao viko mbali kabisa na dini hii tukufu. Hawana hofu ya Mwenyezi Mungu, wanauana na kuwaua watu wasio na hatia. Amiir sahib alitoa mifano kadhaa katika nchi za Pakistan, Bangladesh na Burkina Faso ambao wale wanaonadi kuwa wao ni waislamu safi wanawadhulumu na kuwaua waahmadiyya bila ya sababu za msingi. Aliendelea kusema kuwa kule Burkinafaso kwa mara ya kwanza katika Afrika, waahmadiyya wapatao tisa wameuawa shahidi baada ya wao kukataa kuikana imani juu ya Hadhrat Masih Mau'ud as na hivyo wameonyesha mfano mzuri wa uaminifu, uimara na uthabiti.

Alisema kuwa hii ndiyo hali ya wale wanaodai kwa midomo kuwa wao ni waislamu, ni wajibu wetu kurekebisha hali zetu wenyewe na kisha kurekebisha
hali za watu hao.

Mwisho wa nasaha zake, Amiir Sahib aliongoza maombi ya kimya na kisha kufunga hafla hiyo.

Asemavyo Masihi as - Umuhimu wa Kumfuata Mtume saw

Hazrat Aqdas Masihi Mau›udi a.s anasema: Tazameni, Mwenyezi Mungu Anasema ndani ya Quran Tukufu: Kwa ajili ya kuwa mpendwa wa Mungu Kuna njia moja tu ya ufuasi wa Mtume s.a.w na hakuna njia nyingine yoyote ya kukuunganisheni na Mungu. Lengo la Mwanadamu lapaswa kuwa tu kumtafuta Mungu mmoja Asiye na Mshirika. Yapaswa kujiepusha na shirki na Bidaa. Haipaswi kuzifuata Mila na Kuzitii Tamaa za Nafsi. Tazameni! Ninasema tena kwamba mbali na njia ya kweli ya Mtume wa Allah s.a.w, Mwanadamu hawezi kwa vyovyote vile kufanikiwa.

Mtume wetu ni mmoja tu, na Quran Tukufu moja tu iliyoteremka kwa Mtume huyu, ambayo kwa kuifuata twaweza kumfikia Mungu..... Kumbukeni kwamba hakuna ufunguo mwingine wowote ule wa kufungulia milango ya Fadhili na baraka za Mungu pasipo kufuata maagizo ya Quran Tukufu na Mtume s.a.w na Sala na Saumu, ambazo ndizo njia za SUNNA. Amepotea yule aziachaye njia hizo na kubuni njia yoyote nyingine mpya. Atakufa bila mafanikio yule asiyefuata maagizo ya Mungu na Mtume wake bali anatafuta njia zingine zingine. Malfudhat J. 3, uk. 102 - 103, toleo jipya

MATUKIO KATIKA PICHA

Kufuatia Maazimisho ya Siku ya Masih Aliyeahidiwa[as]



Katibu Mkuu wa Ahmadiyya Tanzania, Seif Hassan NakuchimaSahib akiongoza maombi ya kimya kimya mara baada ya kufunga Mkutano. Kufuatia Maazimisho ya Siku ya Masih Aliyeahidiwa[as] Mijini Dar es Salaam yaliyofanyika Tar. 19-Machi-2023



Kalamu kutoka Kanda ya Ziwa

...Kutoka tolro lililopita

KUCHANUA KWA CHEMCHEM YA JAMAAT AHMADIYYA MKOANI SHINYANGA - 2



Yousuph Mgeleka (Muijukuu)

Mtume SAW alisema: Kuipenda nchi yako ni sehemu ya imani. Naomba sasa niwakilishe nukuu ya ujumbe maalum wa Hadhrat Khalifatul Masih II (ra) Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad kwetu Waafrika kama ifuatavyo:

"Enyi watu wa Afrika! Onyesheni tena dalili ya uadilifu na wema wenu, na toeni msaada kwa kuusimamisha ukweli - ukweli alioutuma Muumba wenu Allah, ambao pasipo kuukubali mataifa yaliyomo utumwani hayawezi kupata uhuru, na wanaodhulumiwa hawawezi kuokoka katika dhulma, na wafungwa hawawezi kutoka katika magereza. Nawafikishieni ujumbe wa Amani, ustawi na maendeleo. Ujumbe huu si wangu, bali ni ujumbe wa Allah ambaye ni Muumba wangu. Huu ni ujumbe wa Allah ambaye ni Muumba wa mbingu na ardhi. Huu ni ujumbe wa Allah ambaye ni Muumba wa Ulaya, Amerika na Asia.

Njooni. Njooni kwa maelfu. Bali njooni kwa Malaki. La, bali njooni kwa mamilioni mkusanyike chini ya bendera ya ukweli, ili sisi sote kwa kuungana pamoja, tuusimamishe tena ufalme wa Allah. Na tusimamishe udugu wa wanaadam ulimwenguni, na tusimamishe uadilifu na wema katika dunia. Allah awapeni nguvu na uwezo wa kuitikia wito wangu, nami nipate kuiona siku ambayo ninyi mtasimama pamoja nami bega kwa bega, tukiendelea na juhudi ya kusimamisha Amani, usalama, maendeleo na ustawi duniani. Na mwishowe, juhudi hii ifanikiwe kwa Baraka na fadhili za Allah. Aamin" – Rabwah, 17.01.1953 (miaka 70 iliyopita).

Mnamo mwaka 2008 mpaka mwaka 2018 hivi, sote tunakumbuka kuwa nchi yetu hii ya Tanzania iligubikwa na wimbi kubwa na ovu la mauwaji katika mikoa ya ukanda wa Ziwa. Mauwaji hayo na ukatili huo yaliyonasibishwa na imani za kishirikina katika jamii nzima na nchi kwa ujumla wake. Kwa kuliona hilo basi na kama nilivyotangulia kutoa hadithi ya Mtume SAW kwamba kuipenda nchi yako ni sehemu ya Imani, basi Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya nchini haikukaa kimya, bali ilipaza sauti na hasa baada ya kuguswa na mauwaji hayo ya kikatili kwa viumbe wenzetu. Hakika, yalikuwa ni mauwaji ya kikatili sana kwa wanaadam wenzetu, nami namuomba Allah awahurumie na awasamehe marehemu wote waliofikwa na mikasa hiyo, na awape nguvu na Imani ya dini ya Islam wale wote waliopoteza viungo vyao dhidi ya ukatili huo.

Kumbe Allah alikuwa amepanga kuiteremshia Jamaat yake fursa njema ya kuitangaza dini aliyoiteremsha duniani, dini ya Kiislam na mafundisho yake kupenyezwa. Naam, Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya (chini ya muongozo wa Amir sahib) na kwa kutambua kuwa eneo fulani katika nchi yetu limezongwa na mauaji ya kikatili kwa Vikongwe, kwa watu wenye ulemavu wa ngozi yaani (albinism) na mengineyo, na hasa mauwaji yalipozidi sana miaka ya 2011 na 2012 ndipo Amir wa nchi yetu Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry aliamua kwa dhati na nguvu zote kuwa Jamaat ijikite katika kuielimisha jamii ya mikoa ya Shinyanga kisha Simiyu na mwishowe Geita kupitia dini ya kiislamu, na kwamba jamii ikielimika katika masuala ya dini basi inshaAllah kutakuwepo na ufaulu mkubwa na kupunguza kama si kukomesha kabisa ukatili huo mkubwa na mauwaji.

Harakati kubwa na za dhati kimahubiri mikoa hii ya ukanda wa Ziwa ikaanza. Na uzuri wake ni kwamba, kiongozi wetu huyu Amir sahib (ambaye mpaka hii leo Allah amejaalia tumeendelea kuwa nae akitulea na kutuongoza hapa nchini) alipoamua kuifanya eneo hili kuwa ni eneo maalum la kimahubiri ili kuinusuru jamii na mauwaji hayo na kisha Jamaat iweze kuchanua na kuwa ni kimbilio sahihi kwa wanajamii wa ukanda wa Ziwa yaani Wasukuma au "wananzengo". Nakumbuka moja ya muongozo rasmi wa Amir sahib ulikuwa ni tujikite zaidi kimahubiri katika mkoa wa Shinyanga kwanza, mkoa ambao ulikuwa ni kinara katika mauwaji hayo ya vikongwe, walemavu wa kawaida na walemavu wa ngozi kuuwawa ndani ya nchi yao, kuuwawa ndani ya maeneo yao, na kuuwawa ndani ya nyumba na makazi yao, jambo hili ilikuwa ni kilio kikubwa sana cha nchi na serikali yetu.

Tunazidi kujionea ya kwamba Mwenyezi Mungu alikuwa na kusudio lake maalum, yaani baada ya miaka 50 ya mahubiri na kutopokelewa kwa Jamaat mkoani Shinyanga kwa upana huo, ndipo Allah akateremsha chemchem kwa jamii hiyo na kushtuka kwa kuona ama kweli hii ni ndio dini kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

i) Dini isiyobughudhi katika maziko.
ii) Dini isiyobughudhi katika uchinjaji.
iii) Dini inayoepusha ushirikina uliotamalaki
iv) Dini inayoelekeza kuabudu bure.
v) Dini inayowaleta watu pamoja kwa upendo na Amani.

Hii ndio Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, huu ndio uzuri wa Jamaat chini ya muongozo wa Ukhalifa. Tukajionea wananzengo wakizidi kupashana kuhusu Jamaat, kwamba jamani dini hii imekuja kwa ajili yetu na kuwa ndio suluhisho la Amani na usalama kwa jamii yetu. Ndivyo ilivyotokea kuwa chemchem hii ya Islam Ahmadiyya kupenya na kuwafikia wananzengo zaidi (yaani jamii ya usukumani) ikiwa na misingi na mafundisho sahihi kabisa ya Uislam wa kweli, uislamu ambao ameufundisha Mtume wetu Muhammad Mustafa SAW. Ama kwa hakika hiki ndicho kiini kikuu cha Jamaat Ahmadiyya kuingia na kupokelewa mkoani Shinyanga. Na kisha Jamaat Ahmadiyya ikaendelea kushamiri hadi kufika katika mkoa wa Simiyu, na kisha kuingia kwa kasi kabisa mkoani Geita, Alhamdulillah. Kazi hii ya kuitoa jamii kutoka kwenye imani za akina Mwanamalundi na kule Gamboshi, haijawahi kuwa ni kazi rahisi wala nyepesi. Ni takriban kila mji ulizingirwa kwa vitu vya shirk, vikichimbiwa chini n ahata kuning'inizwa vibarazani au ndani ya nyumba zao. Upagani ndio ulioshika hatamu kwa kila kitu, huku ulaji wa vibudu ilikuwa ni desturi ya kawaida mno kwa jamii hii. Na kama vile haitoshi huku hamasa ya mahubiri na malezi nchini ikiwa juu kuanzia ngazi ya Jamaat Taifa, basi Majlis Khuddamul Ahmadiyya nao wakakoleza muongozo huu wa Allah kwa ukanda wetu. Pale ambapo walipokuwa safarini wakiongozwa na Sadr MKA wa wakati huo wakagawa vipeperushi maeneo mbalimbali njiani waliposimama na kisha kufika kijiji cha Sungamile na kugawa vipeperushi pia. Kumbe hiyo ikawa ni chemchem nyingine yenye Baraka mkoani Shinyanga na kupekea chanzo kingine cha kuusambaza ujumbe wa Masih Aliyeahidiwa (as) na Jamaat Ahmadiyya mkoani Shinyanga na maeneo jirani.

Ndugu zangu wapendwa na wasomaji wote, Dini ya Kiislam ni Amani. Islam ni Amani. Isingekuwa busara kwa Jamaat Ahmadiyya kuketi kimya huku ikitazama viumbe wa Allah wakiuwana kikatili kabisa kutokana Imani za kishirikina, maamuzi ya Jamaat ilikuwa ni kuwasogezea karibu dini ya Allah na iwe ni ahueni na suluhisho kwa changamoto nzito zilizoikumba jamii nzima ya ukanda huo na nchi kwa ujumla wake. Nyakati hizo zote, nchi iliingia doa kubwa kwa mauwaji yale yenye Imani za kishirikina. Kumbe ndugu zanguni suluhisho la mauwaji yale ilikuwa ni Jamaat Ahmadiyya kuwasili katika mikoa hiyo, hii ndio ilikuwa ni suluhisho ya kweli, maana nakumbuka hata kiongozi mmoja Mkuu ngazi ya mkoa wa Shinyanga alinieleza pembeni kuwa "nyie mmeleta dini na ndio suluhisho la hii hali", akaniambia sisi Serikali tunahitaji mno msaada wenu wa dini kwa jamii). Na hata siku moja katika Mkutano maalum wa Peace Conference uliofanyika mjini Shinyanga mwaka 2014, uliokutanisha viongozi mbalimbali wa madhehebu ya dini, hakika wote waliisifu sana jitihada za Jumuiya katika kuisaidia jamii na kuiokoa na mauaji hayo.

Katika kuona miujiza mikubwa ya Allah na namna Allah anavyobadilisha upepo wa mambo, kazi zile chache za mahubiri na huduma kwa jamii tulizozifanya katika Mkoa wa Shinyanga mwanzoni mwa mwaka 2012, ilipelekea kuanzia Serikali za Mkoa mpaka vijiji (kuitambua na kuishukuru) sana Jamaat Ahmadiyya huku wakitambua na kutamka hadharani kwenye khutba zao mbalimbali kuwa "Nyie Waislamu wa Ahmadiyya mmekuwa ni msaada wetu mkubwa sana katika kuielimisha na kuiweka sawa jamii na wananchi kwa ujumla. Mmetusaidia sana na tunawashukuru sana. Serikali inazitegemea sana dini katika kuielimisha jamii, mnafanya kazi kubwa sana na nzuri mno. Kazi mnayoifanya, inafaa kuigwa na dini na madhehebu mengine".

Kama haitoshi, viongozi hao walikuwa mara kwa mara wakiwasiliana nami (mimi muandishi wa Makala haya) na kutupatia hamasa kubwa kuwa mnafanya kazi kubwa na nzuri sana. Bali kulikuwa pia na mawasiliano kutoka serikali za vijiji, wilaya n ahata mkoa kwenda kwa Mwalimu msimamizi wa mkoa juu ya harakati hizo. Viongozi wa serikali wakazidi kusema kwamba, serikali ipo nanyi na mkihitaji aina yoyote ya msaada basi tupo tayari kushirikiana nanyi. Viongozi hao wakaahidi kuwa Serikali inatambua mno mchango wenu mkubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Shinyanga, na kwamba ipo tayari kushirikiana nanyi wakati wowote ule.

Allah anasema katika Surah Ar-Rahmaan: "Fabiayyi aala irabikumma tukadhibaan - Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?" Hebu tuone matokeo ya jitihada hizi za kuokoa jamii kuteketea kwa kuuwana wenyewe kwa wenyewe kwa Imani hizo za kishirikina:-

1. Leo hatusikii tena matukio ya mauwaji kwa vikongwe mkoani Shinyanga na ukanda wa ziwa.
2. Leo hatusikii tena mauwaji ya ndugu zetu wenye ulemavu wa ngozi mkoani Shinyanga na ukanda wa ziwa.
3. Leo hatusikii tena ndugu zetu wakikatwa viungo kwa imani za kishirikina mkoani Shinyanga na ukanda wa ziwa.
4. Serikali kuu za Mikoa zikaitambua Jamaat Ahmadiyya na kuanza kushirikiana nayo bega kwa bega.
5. Viongozi wa ngazi za Wilaya, kata na hata vijiji wakapewa taarifa na habari za Jamaat Ahmadiyya na kwamba wapewe ushirikiano. Hawa ni Waislamu wema, sio wakorofi.
6. Taarifa zikasambaa sana mkoani Shinyanga, kwamba kuna Jumuiya ya Waislam imeingia huku kwetu, tumeiona Jumuiya hii kuwa ni nzuri na mafundisho yake mazuri. Wanajamii wenyewe wakawa wanapigiana simu toka kijiji kimoja mpaka kijiji cha pili, hali iliyoleta urahisi mkubwa kwa Wahubiri wetu kutekeleza mahubiri kwa wepesi kabla ya kuwafikia wanavijiji wenyewe. Hizi zikawa ni aina nyingine ya Baraka za mahubiri.
7. Jumuiya ikaanza kushirikishwa kwenye vikao muhimu ngazi ya Mkoa hasa inapokuja masuala ya jamii, na Jumuiya ikapewa kipaumbele Zaidi inapojenga hoja zake na kusikilizwa.
8. Jamaat kila inapokwenda na kufanya mahubiri, ikapokelewa kwa mikono miwili Alhamdulillah. Huku baadhi ya wahubiri na Waalim wakikaribishwa kwa wanajamii kukaa kwa siku moja au mbili wakati zoezi la mahubiri likiendelea. Na kukaa huku katika nyumba za wenyeji ilikuwa ni bure kwa kulala na hata chakula pia, yupo hapa katika ukumbi huu wa Jalsa Mzee Shaaban Kalanga anaweza kuthibitisha haya yote na hata Mwl Mbanga au Mwl Kaswezi au Mwl Ramadhan Mahmood sahib anaweza kuthibitisha haya ninenayo, maana tulikuwa wote kwenye kambi mbalimbali katika siku za awali wa mahubiri yetu mkoani Shinyanga.
9. Leo hii Serikali zote za mikoa hiyo inatuthamini sana Jamaat Ahmadiyya, na tunatambulika kuwa ni moja ya Jumuiya zilizoleta suluhisho la kweli kiimani katika jamii zao.
10. Leo hii ukizunguuka vijiji kadhaa basi utakutana na msikiti, ambapo jitihada zetu ziliweza kuwaibua mpaka viongozi na masheikh kadhaa wa madhehebu mengine nao kuona loooh! Hawa makadiani wametuzidi kete na wamefanya jambo kubwa na zuri mno kwa jamii, huku wakisema hawa makadiani wana hela sana sana, na wakisahau kuwa hii ni Jamaat ya Allah.
11. Leo hii unaweza kuzunguuka mikoa hii ya Shinyanga, Geita na Simiyu na kuiulizia Jamaat Ahmadiyya, basi haraka haraka utajulishwa ipo wapi na wapi. Hii ndio Jamaat Ahmadiyya inayoshamiri ukanda wetu. Ndugu zangu wasomaji, inatulazimu baadhi ya nyakati kumshukuru sana Allah kwa kuwa hai na kushuhudia namna Jamaat Ahmadiyya kwa kupitia miongozo ya kimbingu ilivyooweza kupenya na kukomesha na kutokomeza mauaji ya kikati-

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

Sifa za Kipekee na Njema za Kurani Tukufu

Ubora wa Kurani Tukufu – Kutafakari juu ya Neno Kamili la Mwenyezi Mungu

Kutoka uk. 12

Qur'ani Tukufu kwa njia yoyote ile.

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) alimnukuu Imam Ja'far, ambaye inaripotiwa kuwa alisema kwamba alisoma Qur'ani Tukufu kiasi kwamba alianza kufunuliwa Aya zake. Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anaeleza kwamba ingawa hakuna uthibitisho kama kweli alitoa kauli kama hiyo, ukweli ni kwamba inawezekana kabisa kwamba mtu aanze kupata wahyi kupitia baraka za Qur'ani Tukufu.

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) kisha anaeleza kwamba madhehebu mengi ya Waislamu yanatoa maana zao wenyewe za Qur'ani, na hivyo wametoa mafundisho kutoka kwenye Qur'ani Tukufu ambayo si sahihi. Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anasimulia tukio la wakati wa Hadhrat Umar (ra). Wakati fulani, Hadhrat Umar (ra) alikuwa akifanya uamuzi na mwanamke mzee akasema kwamba hii ilikuwa kinyume na kile kilichotajwa katika Hadith. Hadhrat Umar (ra) alisema, "Siwezi kuacha Qur'ani Tukufu kwa ajili ya [kauli ya] mwanamke mzee." Alikazia yale aliyojifunza kutoka kwa maneno ya Mwenyezi Mungu na kuyapa kipaumbele juu ya maneno ya mwanamke. Tusipofanya hivyo, bidaa zitaenea katika Uislamu zitakazotuondoa katika mafundisho yake ya kweli.

Hudhur (atba) alieleza kwamba Waislamu walio wengi sasa wamezama katika ujinga, kwa sababu wanaweza kusoma Qur'ani Tukufu, lakini hawatilii maanani kuifuata. Waislamu walio wengi wanaongozwa na maulama na wanachuoni wa kijina, lakini sisi hatuuoni Uislamu ndani yao, na hiyo ni kutokana na kuichukia kwao Qur'ani Tukufu na bidaa walizoleta ndani ya dini. Pamoja na hayo, bado wanatulaumu sisi Waahmadiyya.

Matendo yanahitajika kwa ajili ya Maendeleo ya Kiroho:

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anaeleza kwamba wale ambao hawaifuati Qur'ani Tukufu kamwe hawataona maendeleo na mafanikio. Mwenyezi Mungu Hajakataza kujishughulisha na kazi za kidunia, lakini hili lisiwe lengo letu. Kusudi letu linapaswa kuwa ni kumwabudu Mwenyezi Mungu na kutenda kulingana na mafundisho yake. Ni kwa sababu hii kwamba amri ya Zakat ipo, ili mali yetu isitimize matamanio yetu ya kidunia tu bali pia ituelekeze kwa Mwenyezi Mungu na imani.

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema kwamba Qur'an ni gunia la vito, lakini watu hawalijui. Watu hawazingatii kwa makini Qur'an kama wangezingatia mambo mengine. Kulikuwa na mshairi katika Batala aliyekuwa anaandika ushairi wa Kiajemi. Aliandika ubeti wa kwanza, kisha akahuzunika sana kwamba hakuweza kupata ubeti wa pili unaofaa. Alienda kwa fundi cherehani na kupoteza muda wake maana akili yake ilikuwa kwenye ushairi wake, na baada ya kuzomewa na fundi cherehani kwa kumpotezea muda, aliweza kuandika ubeti wa pili alioridhika nao. Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anaeleza kwamba hatutumii juhudi sawa na mshairi huyu katika kuielewa Qur'ani Tukufu, hata hivyo tunapaswa.

Kisha Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema kwamba pale Qur'ani Tukufu inapotoa amri, pia inatoa uthibitisho na ushahidi wa manufaa ya amri hiyo. Hakuna udanganyifu na uwongo unaoweza kusimama mbele ya Qur'ani Tukufu, na ni kwa sababu hii kwamba mtu yeyote ambaye ni mwongo hawezi kusimama dhidi yetu, hata katika mazungumzo. Tumebarikiwa kupitia Qur'ani Tukufu kwa maarifa yasiyoweza kupingwa.

Zaidi ya hayo, Hudhur (atba) alimnukuu Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as), aliyeeleza kwamba kwa kushikamana na Qur'ani Tukufu, tunaweza kumpata Mwenyezi Mungu. Anasema tuna nabii mmoja ambaye juu yake mafundisho haya kamili yalifunuliwa. Siku hizi, wengi hufuata njia za mafumbo na kujiingiza katika maombi ya jadi, hata hivyo, njia hizi zitatuondoa kwenye njia sahihi. Ni lazima tumfuate Mtume Mtukufu (saw) aliyedhihirisha mafundisho kamili ya Qur'ani Tukufu, na hapo ndipo tutakapopokea ufunguo wa kufungua mlango kwa Mwenyezi Mungu.

Maandiko Yanayowaunganisha Watu wote:

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema kwamba Qur'ani Tukufu ilileta amani kati ya watu wote kwa sababu inaifanya imani ya Mitume wote kuwa ni wajibu kwa wanadamu. Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) pia alitoa changamoto kwa mtu yeyote kuleta kitabu kinachoimarisha amani kwa mtindo huo huo. Qur'ani Tukufu pia ina sifa ya kuwa na utaratibu unaoongeza ufasaha na usemi wake. Kitu ambacho hakina utaratibu wowote hakiwezi kuwa fasaha, hata hivyo, Qur'ani Tukufu iko katika mpangilio kamili, inatumia lugha nzuri na haiachi chochote wakati wa kufafanua jambo. Hata wale ambao ni wa kupindukia katika kuonyesha utaratibu mara nyingi hushindwa kufuata utaratibu. Qur'an Tukufu, kwa upande mwingine, ina mizani isiyoharibika na ni kamilifu, na kwa sababu ni neno la Mwenyezi Mungu, ni lazima iwe fasaha.

Miujiza miwili ya Qur'ani Tukufu:

Huku akitaja miujiza miwili ya Qur'ani Tukufu, Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema kwamba Umma wa Kiislamu umepewa miujiza miwili. Mwujiza wa kwanza ni maneno halisi ya Qur'an Tukufu ambayo ni kamilifu na yenye ufasaha usio na kifani. Mwujiza wa pili ni athari na uwezo wa Qur'ani Tukufu. Lau uwezo na athari za Qur'an zingekosekana, Umma wa Kiislamu ungenyimwa dalili na miujiza mingi ambayo imetolewa.

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema zaidi kwamba wale wanaoifuata Qur'ani Tukufu wanaanza kupata wokovu duniani tu. Qur'an Tukufu inamtakasa mtu kutokana na makosa yao na kuwaondolea mashaka na udhaifu wao wote. Maneno yake yamekamilika kwa elimu ya hakika na maarifa kiasi kwamba mashaka yoyote katika mioyo ya watu yanaweza kuondolewa nayo, hata hivyo, ili kufaidika nayo ni lazima tujitahidi kuielewa.

Qur'ani Tukufu ina nuru yote ambayo ni muhimu katika kukabiliana na giza la wakati huu. Mafundisho yake yanang'aa kama jua, na ina tiba ya magonjwa yote ya kiroho ndani yake. Hakuna mwongozo wa Mwenyezi Mungu ulioachwa ndani yake, na mwenye kuufuata husafisha moyo wake kikamilifu na huweka muungano na Mwenyezi Mungu. Baada ya hapo, mtu huanza kupata uzoefu wa kuwepo kwa Mwenyezi Mungu na katika wakati wa shida, maombi yao yanajibiwa na Mwenyezi Mungu. Hata mtu akiomba mara elfu katika matatizo yake, Mwenyezi Mungu Humjibu mtu kama huyo kwa upendo mara elfu. Kupitia mafundisho yake, mtu huoshwa na udhaifu wote wa kibinadamu na kujazwa na usafi.

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) kisha anaeleza kwamba hatuna kitabu kamili zaidi kisicho na shaka yoyote. Anasema tena kwamba mwanzoni, Mwenyezi Mungu Alituma muongozo kwa kila umma kando kando. Kisha, alipotaka wanadamu waunganishwe ili kuakisi umoja Wake, Aliteremsha Qur'ani Tukufu. Aliunganisha mataifa, watu na lugha za wanadamu kupitia Qur'ani Tukufu.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba siku hizi, tunaona haya yakitokea katika mtazamo wa kidunia kwa sababu dunia sasa imekuwa kama kijiji cha kimataifa. Hata hivyo, tumeunganishwa katika lugha kupitia Qur'ani Tukufu kwa sababu tunatumia lugha ya Kiarabu katika sala zetu, bila kujali tunatoka taifa gani.

Hisani ya Kurani Tukufu Juu ya Maandiko na Manabii Waliotangulia:

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anaeleza kwamba Qur'ani Tukufu imefanya ihsani kubwa kwa mafundisho na Mitume wa zamani kwa sababu imegeuza masimulizi yao ya hadithi kuwa ni mafundisho ya kielimu. Hivyo, hadithi za mitume wa zamani haziwezi kueleweka kikweli bila kusoma Qur'ani Tukufu. Watu wanatupinga sisi na mafundisho ya Qur'ani Tukufu ni kwa sababu hii kwamba tunataka kuyawasilisha kwa jinsi yalivyoteremshwa na Mwenyezi Mungu.

Utukufu wa Qur'ani ni katika ukweli kwamba ina mafundisho ambayo hayapatikani popote katika Taurati na Injili, na tunaweza tu kujifunza mafundisho haya ikiwa tutasoma na kuzama ndani ya Aya za Qur'ani Tukufu.

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) alieleza kwamba Qur'ani Tukufu imejaa mwongozo na amri kutoka kwa Mwenyezi Mungu zinazotusaidia sisi tujiboreshe zaidi. Hivyo, tunapoisoma Qur'ani Tukufu, tunapaswa kutafuta mwongozo huu na kutenda kulingana na amri tunazozipata humo.

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anaeleza zaidi kwamba Qur'ani Tukufu haina maoni yoyote ya wanadamu na ni kamilifu katika mambo yote kwa sababu imetoka kwa Mwenyezi Mungu Mwenyewe. Kwa hakika Mwenyezi Mungu Amehesabu kila herufi yake. Kwa hivyo, imelindwa dhidi ya kubadilishwa. Tunaona kwamba mafundisho ya Qur'ani Tukufu na maana zake za ndani bado ziko sawa hata leo.

Maana Mpya za Qur'ani Tukufu Zinajidhihirisha zenyewe Kulingana na Uhitaji wa Zama:

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema zaidi kwamba Qur'ani Tukufu inadhihirisha mafundisho yake kulingana na uhitaji wa zama. Katika zama hizi, kwa sababu kuna nguvu nyingi za Dajjali na njama nyinginezo za kuwapotosha wanadamu, basi kutoka kwa Mwenyezi Mungu tunapata mwongozo unaohitajika wa kupambana na nguvu hizi ndani ya Qur'ani Tukufu. Hivyo, mwongozo huu unaweza kuwa umefichwa kwa wale waliokuwa kabla yetu, lakini sasa, umedhihirika. Qur'ani Tukufu ni kitabu ambacho kitaendelea kuwepo hadi Siku ya Hukumu kwa sababu kina uwezo wa kupata mafundisho kulingana na uhitaji wa zama.

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anaendelea kusema kwamba mafundisho haya na elimu hayatoki ndani ya Qur'ani Tukufu bila sababu, badala yake, yanadhihirika kwa wakati mkamilifu na wakati yanapohitajika zaidi.

Hudhur (atba) alisema kwamba mtu asifikirie kwamba amejifunza Qur'ani nzima baada ya kuisoma. Badala yake, baada ya kuisoma na kuisoma mara moja, tunapaswa kuisoma tena na tutaona kwamba ujuzi wetu umekomaa na kile tulichokuwa tumejifunza hapo awali kilikuwa ni ufahamu wa msingi sana. Hivyo, mtu ataendelea kujifunza na kuendelea mwaka baada ya mwaka ikiwa atasoma Qur'ani Tukufu kwa namna hii.

Elimu ya Qur'ani Tukufu huwafungukia tu wale walio safi na wacha-Mungu, na wanaoisoma kwa moyo ulio wazi. Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alitaja kwamba Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) alipewa ufahamu mkubwa wa Qur'ani Tukufu, na inatupasa tuisome kwa nuru ya maandishi yake ili kupata ufahamu wa ndani zaidi wa maana zake.

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anaeleza kwamba Qur'ani Tukufu ina mwongozo kwa watu wa ngazi zote za ufahamu. Wengine wanaweza kuwa na uwezo mdogo kuliko wengine, hata hivyo, hawajanyimwa nuru ya Qur'ani Tukufu. Ina mafundisho kwa watu wote na kwa nyakati zote zijazo. Ukuu wa Qur'ani Tukufu unaweza kuthibitika tu duniani ikiwa tutaifuata, na ni lazima tufikishe elimu yake kwa wengine.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) kisha anamnukuu Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anayesema kwamba wale ambao ni watenda dhambi wataangamia. Ni kwa sababu hii kwamba Mwenyezi Mungu Ametuma mitume na mafundisho yake, ili wanadamu waweze kuokolewa na maangamizo. Katika suala hili, Qur'ani Tukufu inatimiza kikamilifu lengo hili la kuwaokoa wanadamu na kuwaongoza kwenye wokovu. Wale wanaoiacha Qur'ani na Mtume Mtukufu (saw) ni watu wa motoni.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba ni vipi mtu mwenye imani kama Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anaweza kuuvunjia heshima Uislamu na Mtume Mtukufu (saw)? Mwenyezi Mungu Awawezeshe wengine kulielewa hili pia. Waislamu waepushwe na mitego ya maulamaa wa Kiislamu na wamtambue Imam wa zama.

Njia Ambayo Kwayo Mwenyezi Mungu Anailinda Qur'ani Tukufu:

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema kwamba Mwenyezi Mungu Ameahidi Mwenyewe kuilinda Qur'ani Tukufu. Hii ina maana kwamba mafundisho ya Qur'ani Tukufu yanapoeleweka vibaya au kufasiriwa vibaya, Mwenyezi Mungu Atamteua mtu ambaye ataeneza mafundisho ya kweli ya Qur'ani. Kwa mujibu wa ahadi hii, Mwenyezi Mungu Alimtuma Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as).

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema kwamba ni muhimu tuangalie hali ya wakati wetu. Dajjal anajaribu kuipotosha dunia kutoka kwenye dini, na Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) amefika ili kupambana na nguvu hizi. Hivyo, badala ya kumlaumu, ni lazima watu watambue mahitaji ya zama hizi.

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anaeleza kwamba madhumuni ya Qur'ani Tukufu ni kutubadilisha kutoka kuwa hali ya wanyama kwenda kwa wanadamu, na kutoka kwa hali ya wanadamu kwenda kwa wanadamu wenye khulka njema. Zaidi ya hayo, inatugeuza kutoka kwa hali ya wanadamu wenye khulka njema hadi kuwa wanadamu wanaomcha Mwenyezi Mungu.

Hudhur (atba) alitaja kwamba Myahudi mmoja alimwambia kwamba ingawa yeye si Mwislamu, yeye anaamini Mtume Mtukufu (saw) kuwa ni Mtume wa kweli. Sababu ni kwamba hali ya mabedui wa Uarabuni ilikuwa ya kusikitisha, na baada ya ujio wa Mtume Mtukufu (saw) na kuteremshwa kwa Qur'ani Tukufu, walibadilishwa kabisa.

Huku akiwausia umma wake kushikamana na Qur'ani Tukufu, Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) ameweka sharti la sita katika masharti ya Bai'at. Anasema kwamba mwenye kuweka kiapo cha utii kwake atajiepusha na kushikamana na mila na desturi na atashika amri za Mtume Mtukufu (saw) na Qur'ani Tukufu. Hakuna Chochote Kinachoweza Kuongezwa au Kupunguzwa kutoka kwenye Qur'ani Tukufu.

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anaeleza zaidi kwamba hatuwezi kubadilisha chochote kutoka ndani ya Qur'ani Tukufu wala kuongeza juu yake. Wale wanaojaribu kufanya hivyo au kututuhumu kufanya hivi wanapaswa kuleta uthibitisho, kwa sababu sisi ni watu tunoashikamana kikamilifu na yale ambayo Mtume Mtukufu (saw) ametufundisha. Mtume Mtukufu (saw) hakuongeza, wala hakupunguza kutoka katika mafundisho ya Qur'ani Tukufu, na sisi tunamfuata yeye. Ikiwa tungefanya hivyo, basi bila shaka tungekamatwa.

Mwishowe, Hudhur (atba) aliomba kwamba Mwenyezi Mungu Awawezeshe Waahmadiyya wote kuielewa Qur'ani Tukufu na kunufaika na mafundisho yake.

Kukumbusha Maombi kwa Waahmadiyya nchini Burkina Faso na Bangladesh:

Mbali na hayo, Hudhur (atba) aliwataka Waahmadiyya wote kuwaombea Waahmadiyya wa Pakistani na pia kuiombea hali ya nchi hiyo. Aidha aliwakumbusha wanajumuiya kuwaombea dua Waahmadiyya wa Burkina Faso na Bangladesh ambako Masheikh wa Kiislamu wanawasababishia matatizo. Hudhur (atba) aliomba kwamba Mwenyezi Mungu Awawezeshe Waahmadiyya wote kufaidika na mwezi ujao wa Ramadhani na kunufaika na mafundisho ya Qur'ani Tukufu.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

RAMAZAN-SHAWAL.1444AH | APRILI 2023 | ZAHOOR 1402 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufusaw

Abu Huraira*ra* anasimulia kwamba: Nilimsikia Mtume*saw* akisema: Abu Huraira wallahi mimi naomba msamaha kwa Allah kutubia kwake kwa siku moja zaidi ya mara sabini (**Bukhari**).

Sifa za Kipekee na Njema za Kurani Tukufu

Ubora wa Kurani Tukufu – Kutafakari juu ya Neno Kamili la Mwenyezi Mungu

بسم الله الرحمٰن الرحيم

Sifa za Kipekee na Njema za Kurani Tukufu
Ubora wa Kurani Tukufu – Kutafakari juu ya Neno Kamili la Mwenyezi Mungu:

Baada Ya Kusoma Tashahhud, Tawwudh na Surah Al Fatiha Hadhrat Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih wa Tano (atba) alisema kwamba ataongea kuhusiana na hadhi ya kweli ya Kurani Tukufu.

Qur'ani Tukufu Inaeleza Makusudio ya Dini kwa Kweli:
Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alimnukuu Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) aliyeeleza dini ni nini hasa kwa mujibu wa Qur'ani Tukufu na athari zake kwa wanadamu. Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema kwamba Injili hazielezi ni nini athari ya dini kwa wanadamu, hata hivyo, Qur'ani Tukufu inaeleza kwamba dini haina lengo la kumwonyesha mtu dhaifu kama mtu mwenye nguvu. Badala yake, kusudi la dini ni kumwongoza mwanadamu kutumia uwezo na nguvu alizopewa na Mwenyezi Mungu kwa wakati na mahali panapofaa. Dini haina uwezo wa kubadilisha sifa za asili, lakini inasaidia tu kudhihirisha sifa hizo kwa nyakati zinazofaa. Dini haisisitizi matumizi ya rehema wala msamaha, bali inasisitiza usawa wa sifa hizo.
Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) alieleza kwamba mtu asiyetenda vitendo vinavyofaa kwa wakati na mahali sahihi hufanya makosa. Kwa mfano, ikiwa mtu mwenye mamlaka anaendelea kuwatendea wengine kikatili huku anaonyesha nguvu yake ndiye anayekosea. Nguvu au sifa zake si mbaya, bali matendo yake ni mabaya.

Tiba kwa Magonjwa Yote:
Zaidi ya hayo, Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anaeleza kwamba moja ya makusudio ya ujio wake ni kuthibitisha ukweli wa Qur'ani Tukufu. Anasema kwamba wale ambao ni Waislamu hawaielewi Qur'ani kutumika kwa wakati mwingine. Ni Qur'ani Tukufu pekee iliyo na tiba ya magonjwa yote, na mafundisho ya kukuza sifa nzuri. Kwa hivyo, lazima tuifuate.



*Hadhrat Ameerul Mumineen Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih wa Tano*atba *akihutubia waaminio Ijumaa katika Masjid Mubarak, Uingereza Tarehe 17 Machi, 2023. Akieleza Sifa za Kipekee na Njema za Kurani Tukufu Ubora wa Kurani Tukufu – Kutafakari juu ya Neno Kamili la Mwenyezi Mungu*

Tukufu, na sasa Mwenyezi Mungu Ametaka kuonyesha maana za kweli za Qur'ani Tukufu. Mafundisho ya Qur'an ni ya namna ambayo hakuna anayeweza kuyapinga, na ni makamilifu kiasi kwamba hata wanafalsafa hawawezi kupata kosa ndani yake.
Huku akiiusia Jamaat yake kutafakari juu ya Qur'ani Tukufu, Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema kwamba Qur'ani ina maelezo ya mema na mabaya yote, pamoja na bishara kuhusu mustakabali na elimu nyigine nyingi. Qur'ani Tukufu inawasilisha dini isiyo na dosari na ambayo kwayo mtu anaweza kupata baraka. Injili hazijakamilisha dini. Kwa kiasi kikubwa, mafundisho ya Injili yalihitajika kulingana na wakati wa Nabii Isa (as), lakini hayawezi

Uhitaji wa Kutafakari Juu ya Qur'ani Tukufu:
Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anaendelea kusema kwamba tunapaswa kuepuka kujihusisha katika njia mbalimbali za kimila za maombi na badala yake tuutumie wakati huo kwa ufasaha zaidi katika kuitafakari Qur'ani Tukufu.
Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba baadhi ya watu wanajihusisha na njia za kimila za kuomba bila kujua maana halisi ya kile wanachoomba. Badala yake, ingefaa zaidi kutumia muda huo katika kutafakari juu ya Qur'ani Tukufu. Hiyo italeta maendeleo ya kiroho. Waislamu wasiokuwa Waahmadiyya wameleta uzushi na bidaa nyingi katika imani kutokana na hili, na baadhi ya Waahmadiyya pia wameathiriwa. Hivyo, ni lazima tuzingatie zaidi kusoma na kutafakari juu ya Qur'ani Tukufu.
Hudhur (atba) alisema kuwa wiki ijayo, Ramadhani itaanza. Sisi sote tunapaswa kutilia maanani sana usomaji wa Qur'ani Tukufu.
Hadhrat Khalifatul Masih (atba) kisha akamnukuu Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as), aliyesema kwamba kama moyo wa mtu ni mgumu, basi unaweza kulainika kupitia Qur'ani Tukufu. Popote pale inapotajwa dua fulani, mwaminio huomba dua hiyo hiyo kwa ajili yake. Qur'an Tukufu ni sawa na bustani, ambamo mwaminio hung'oa ua kutoka sehemu moja, kisha anaenda sehemu nyingine na kujichumia ua jingine. Hivyo, lazima tufaidike na kila nafasi inayopatikana katika Qur'ani Tukufu ili tuweze kupata maendeleo ya kiroho. Pale ambapo Qur'ani Tukufu imetuagiza kuonyesha khulka fulani njema, tunapaswa kufanya hivyo, na pale Qur'ani inapokataza kitendo fulani kiovu, tunapaswa kujizuia sisi wenyewe kufanya hivyo.

Njia Mbili ambazo Kutokana nazo Mtu Ananyimwa Baraka za Qur'an Tukufu:
Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) kisha anaeleza njia mbili ambazo mtu anakuwa mbali na Qur'ani Tukufu. Njia hizo mbili ni wazi na za siri. Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anaeleza kwamba mtu anaonyesha chuki kwa Qur'ani Tukufu kupitia matendo yake. Tunapoonyesha chuki ya kimwili kwa Qur'ani Tukufu, ina maana kwamba hatusomi kabisa. Waislamu wengi sasa wanafanya hivi, na licha ya kujiita Waislamu, hawajui kabisa Qur'ani Tukufu. Njia ya pili ambayo mtu anaonyesha kuchukia Qur'ani Tukufu ni kwamba hafaidiki na mwongozo na baraka zake, licha ya kuisoma. Hivyo, tunapaswa kujaribu kujiokoa kutokana na kuchukia

Endelea uk.11



Imeandikwa katika Swali & Muundo wa majibu, muhtasar huu lakini kitabu cha kina kinatafuta kutoa maelezo ya msingi ya Imani ya Kiislamu ya Ahmadiyya na yake mazoea.

Pia inatoa habari fulani kuhusu Ahmadiyyat katika Afrika Mashariki.

Nakala hii itapatikana kwa Sh. 3,300/=

Je, Wajua?

Je, wajua kuwa mwaka 1969 binadamu wa kwanza alikanyaga katika Ardhi ya Mwezi katika safari ya siku tatu ya kwenda mwezii. Watu watatu walisafiri safari hiyo.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie
mapenziyamungu36@gmail.com